
ama

AFYA NA MAZINGIRA

Kinababa wanavyotapeliwa biashara ya kuwapa ujauzito wahitaji India

Mbadala wa elimu uliyorahisisha vita vya bangi kwa vijana Arumeru

Staili ya Rais kuwekeza PPP ndani safari inayoipaisha Sekta ya Afya

•Darasa kutoka NHIF, hospitali kukaa meza moja

UKURASA 11

**BENKI** NMB, SMZ zazindua mikopo boti za uvuvi Z'bar

UKURASA 5

**DIWANI,** wenzake mbaroni TAKUKURU tuhuma za kuuza shamba la wizara

UKURASA 7



UKURASA 8

**MAKALA MAALUM**

Mkasa wa 'Treni ya Mwekyembe kuondoa abiria saa saba usiku


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Alhamisi Januari 11, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581552

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Mvua yatikisa, yaacha maafa

**FAMILIA** yaangamia, baba ajinusuru juu ya mti ... *Endelea ukurasa 2*






Wananchi wakiangalia nyumba ya Daines Muruto iliyoanguka katika kata ya Mtii, wilayani Same, mkoani Kilimanjaro jana, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha na kusababisha kifo cha mfanyakazi wake, Joel Gilbert. **Picha juu:** Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, wakishirikiana na wananchi wa eneo la Lukuyu, kumtafuta Mwanahamisi Issa (35) kwenye Mto Mgolole, baada ya familia nzima kusombwa na maji. **PICHA: MARY MOSHA NA CHRISTINA HAULE**

# Maradhi yasiyoambukiza yamshtua Samia

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Waziri wa Afya wa Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, baada ya kuzindua Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mjini Magharibi 'Lumumba', Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**



## Mjamzito aliyebakwa avimba tumbo, miguu, waziri atoa maagizo

UKURASA 4

**MICHEZO** AMROUCHE AWATAKA WACHEZAJI STARS KUJITUMA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana (kulia), akisalimiana na baadhi ya viongozi wa dini mkoa wa Singida (kutoka kushoto), Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Syprian Hilinti na Sheikh wa mkoani humo, Issah Nassoro walipokutana kwenye uzinduzi wa kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mvua yatikisa, yaacha maafa

**Na Waandishi Wetu**

MVUA iliyonyesha maeneo mbalimbali nchini imesababisha maafa yakiwamo vifo na uharibifu wa mali.

Katika maafa hayo, watu wanne wa familia moja wakifariki dunia na mwingine kuokolewa baada ya kusombwa na maji na mafuriko yaliyojaza Mto Mgolole, Kata ya Bigwa, Manispaa ya Morogoro.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Mrakibu (SF) Shabani Marugujo, alisema mafuriko hayo yalitokea usiku wa kuamkia jana kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha mkoani humo.

Aliwataja waliokufa maji kuwa ni Theresia Adolph (73), Asnati Thomas (6) na Mwanahamisi Issa (35) ambaye mwili wake bado unaendelea kutafutwa kwenye mto huo. Miili ya marehemu hao imehifadhiwa katika chumba cha maiti Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro baada ya kuopolewa kwenye tope.

Marugujo alisema baba wa familia hiyo, Sengo Hamisi (47), alijiokoa na kutoa taarifa na sasa katika Kituo cha Afya cha Mgolole kwa matibabu.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Mtaa wa Lukuyu, Edmund Masamba, alisema mvua ilianza kunyesha juzi majira ya saa 4:00 usiku na ilipofika saa 10:00 alfajiri, alipigiwa simu kuwa kuna familia ilikuwa inajaribu kujiokoa lakini imesombwa na maji ya mto huo.

Masamba alisema huenda watu hao wasingepatwa na mauti kama wangekaa ndani sababu nyumba yao bado ni nzima na vyombo vyao vikiwamo vistuli, makochi na vitanda bado vimo ndani.

Majeruhi wa tukio hilo, Hamisi, alisema akiwa ndani kwake saa 7:00 usiku, akitaka kwenda kujisaidia, alikutana na maji yakiwa yameingia ndani kidogo na kuamua kuwaamsha wenzake waliokuwa wamelala ili watafute sehemu ya kutulia kupisha mafuriko hayo.

Alisema akiwa nje na familia yake, waliamua kuzunguka nyuma ya nyumba na kujaribu kuvuka kwa pamoja sehemu ya mto iliyokuwa ikipita lakini walishindwa, hivyo kusombwa na maji hadi bondeni ndipo alipopanda juu ya mti na kukaa hapo kwa saa nne hadi maji yalipopungua.

Hamisi alisema asubuhi maji yalipungua ndipo akashuka kwenye mti na kuanza kupiga kelele akiomba msaada wa kutafuta wenzake na yeye alipelekwa hospitalini kwa matibabu kwa sababu alikuwa amekunywa maji machafu.

Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdul Aziz Abood, aliwataka wananchi wanaoishi kwenye maeneo hatarishi hasa pembeni mwa mito kuchukua tahadhari huku wakizingatia kanuni za uhifadhi wa mazingira kwa kupanda miti.

**MAAFA SAME**

Mvua inayoendelea kunyesha Same mkoani Kilimanjaro, imesababisha vifo vya watu wawili, kukata mawasiliano ya barabara za Tarafa za Miamba na Gonja.

Athari zingine zilizosababishwa na mvua hiyo ni pamoja na ekari 120 za mpunga kusombwa na maji huku takriban nyumba 15 zikiingiliwa na maji.

Akizungumza baada ya kutembelea tarafa hizo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema kata zilizoathirika na mafuriko hayo ni kata ya Bombo, Mtii, Maore, Kalemawe, Ndungu na Lugulu.

Babu alisema miongoni mwa sababu zilizofanya kuwapo maafa hayo ni uharibifu wa mazingira kutokana na wananchi kulima katika maeone yenye maporomoko na kukata miti ovyo, hivyo kuwaonya wananchi kuacha kufanya shughuli za kilimo katika maeneo hayo.

"Nitoe agizo watu waache kulima pembezoni mwa barabara na vyanzo vya maji na maeneo yenye mteremko kwa sasa kunahali nzuri ya hewa pandeni miti ya kutosha. Yeyote atakayebainika kukata miti ovyo hatutamvumilia," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni, aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Noel Gilbert (17) mkazi wa Mtii na mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Lugulu, Ramadhani Ayubu (12).

Mmoja wa wananchi, Mwanaisha Juma, aliomba serikali kuwapa elimu ya namna bora ya kulima kilimo cha matuta kinachoweza kusaidia mmomonyoko wa udongo.

Diwani wa Bombo, Philemon Msuya, alisema bado wananchi wa kata za milimani wanajenga makazi kwa mazoea, hivyo na kuiomba Halmashauri ya Wilaya ya Same kutoa elimu kabla ya watu kuanza ujenzi.

**Imeandikwa Christina Haule, (MORO) na Mary Mosha SAME)**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
09.01.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **13.01.2024 hadi 20.01.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Bandari ya Dar Es Salaam** kuelekea **Mzenga, gari** hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB15200 DS00TG GP / NRB43293**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **36.50** |
| **Upana** | - | **Mita** | **7.40** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.70** |

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar Es Salaam** hadi **Mzenga** kupitia **Barabara ya Mandela,** Barabara ya Morogoro mpaka Mlandizi, magari yatasafiri muda wa usiku ***( Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri).*** Kutoka Mlandizi kwenda Mzenga magari yatasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117781502

## Kasi maradhi yasiyoambukiza yamshtua Samia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza ni kubwa, hivyo halitoi taswira nzuri katika sekta ya afya.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua Hospitali ya Rufani ya Lumumba, Mkoa wa Mjini Magharibi ambayo imejengwa kutokana na fedha za UVIKO-19 zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa kupitia serikali ya Tanzania.

Rais alisema vifo vinavyotokana na magonjwa hayo vimeongezeka kwa asilimia 14 kutoka milioni 2.6 mwaka 2019 hadi milioni 3.1 mwaka 2023.

Magonjwa hayo, alisema yanachangia asilimia 33 ya vifo vyote ikimaanisha kwamba kati ya watu watatu, mmoja ana ugonjwa usioambukiza kama vile kisukari, uzito uliopitiliza, shinikizo la damu na maradhi ya moyo.

Kutokana na ongezeko la maradhi hayo, kila mmoja kwa nafasi yake kuzingatia ushauri wa wataalamu kufanya mazoezi na kula vyakula vinavyozingatia mlo kamili.

Pia alisema licha ya moja ya malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa kutoa huduma za matibabu bure, kwa sasa ni vyema wananchi wakachangia huduma hiyo.

Alisema suala la kuwa na bima ya afya kwa sasa haliepukiki ili wananchi wapate huduma bora badala ya kuendelea kusubiri kupata matibabu bure, hivyo kuiachia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuangalia sera na mipango yake lakini kwa upande wake, suala la bima afya haliepukiki.

"Wako watakaosema hiyo si dhamira ya Mapinduzi watu kuchangia huduma za afya. Sasa tuchague, tuchangie huduma za afya au tufe na hapa tulipofika na huduma za afya ziende chini?" alisema.

Rais Samia alisema zinatumika gharama kubwa za miundombinu ya huduma za afya, hivyo wasipochangia itasababisha huduma hizo kurudi nyuma.

"Ili matibabu yaendelee ni gharama kubwa na kuiachia serikali ibebe mzigo wote si rahisi. Tumejenga miundombinu mizuri, vifaa vya kisasa lakini tusipochangia huduma zitarudi nyuma na itakuwa kazi tuliyoifanya ni bure," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi kutunza miundombinu ya hospitali hiyo ili idumu kwa muda mrefu huku akiwataka watoa huduma kutoa huduma bora.

"Kuwa na majengo ni jambo moja lakini huduma inayotolewa ndani ni jambo lingine. Kwa hiyo ndugu zangu tuzingatie hili na Wizara ya Afya hakikisheni mnalisimamia," alisisitiza.

Rais aliwataka watoa huduma wa hospitali hiyo kutoa huduma nzuri na kutumia lugha nzuri kwa wagonjwa wanaowahudumia.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kutokana na uboreshaji wa afya kwa sasa kuna vitanda 2,645 kutoka vitanda 1,445 vya awali.

Alisema kulikuwa na chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) kimoja chenye vitanda vinane sasa kuna ICU 14 zenye vitanda 80 na kilikuwa na vyumba vya upasuaji 11 kwa sasa viko 35 na kutoka dharura moja kufikia 13.

"Hii ni hospitali ya hadhi kubwa ikiwa na ICU nne. Tulikuwa tunatumia gharama kubwa kupeleka wagonjwa nje sasa itapungua," alisema.

Mazrui alisema wakati Hospitali ya Rufani ya Mnazimmoja inayotegemewa kuvunjwa mwaka huu kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati mkubwa, kwa sasa Lumumba ndiyo itakuwa mbadala wake.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Amour Suleiman Mohamed. alisema hospitali hiyo imegharimu Sh. bilioni 32.5 ikijumuisha vifaa na ununuzi wa magari mawili ya wagonjwa.

Alisema hospitali hiyo itakuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa 893,000 kutoka shehia 121 na itakuwa na uwezo wa kulaza wagonjwa 220 kwa wakati mmoja.

"Itatoa huduma za kibingwa, uchunguzi maradhi tofauti, wagonjwa wa ndani, wajawazito, wodi ya wagonjwa wenye mahitaji maalumu na vyumba vinne vya wagonjwa mahututi," alisema.

# CHADEMA: Miswada sheria za uchaguzi iondolewe bungeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeshauri kuondolewa bungeni kwa miswada minne ya sheria zinazohusu uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), badala yake kuwasilishwe muswada wa marekebisho ya Katiba ya nchi.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, aliwasilisha hoja hiyo jana alipotoa mapendekezo ya chama chake mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu miswada ya sheria hizo.

Alisema miswada hiyo ya sheria za uchaguzi bado ina upungufu mwingi ambao unastahili kufanyiwa marekebisho na suluhisho kuu ni mabadiliko ya Katiba.

"Ni heri miswada hii yote ikaondolewa na kuletwa muswada wa sheria ya mabadiliko ya Katiba," alisisitiza Mnyika, akisema CHADEMA haikubaliani na muundo wa NEC uliopendekezwa kwenye muswada wa sheria.

"Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi uliopendekezwa kwenye sheria unaeleza tume hiyo, kuwa kwa kiasi kikubwa itakuwa ni ya Rais wakati na yeye pia ni mgombea," alisema Mnyika.

Alisema wanapendekeza wajumbe wa tume hiyo badala ya kuteuliwa na Rais ni lazima wapite kwenye kamati ya uteuzi ambayo itajumuisha uwakilishi wa makundi mbalimbali.

Alisema pia wanapendekeza Sheria ya Uchaguzi imwondolee Rais mamlaka ya kuteua Mkurugenzi wa NEC, bali kuwe na tume huru ndiyo yenye jukumu hilo. CHADEMA inapinga matumizi ya wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi.

"Serikali yetu lazima itekeleze uamuzi wa Mahakama ya Afrika ambayo iliagiza kuondolewa kwa wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi mbalimbali.

"Watu wanakuwa wabishi kuhusu suala hili kwa madai kuwa wakurugenzi ni waaminifu. Uaminifu gani walionao ilhali ripoti za CAG ambazo zimekuwa zinatoka mara zote zinaonesha ni kwa namna gani walivyo wabadhirifu?" alihoji Mnyika.

Alisema ili kuondokana na shida hiyo, NEC inapaswa kuajiri watumishi wake binafsi ambao itawatumia katika shughuli zake wakati wote.

Mnyika alisema CHADEMA inapendekeza kuondolewa kwa kifungu kwenye muswada wa sheria ya uchaguzi ambacho kinapiga marufuku chama kuingiza vifaa vya kampeni kutoka nje ya nchi siku 90 kabla ya uchaguzi.

"Kwa sheria hii hata chama kikitaka kuingiza hata helikopta ya kufanyia kampeni, hakiwezi! Tunapendeza kifungu hiki kiondolewe kwenye sheria hii," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Joseph Mhagama, alisema vyama vyote vimepewa nafasi sawa kwenye kutoa maoni.

"Tumewapatia nafasi sawa ambapo taasisi za dini ilikuwa ni dakika 30, vyama vya siasa dakika 20, mashirika dakika 10 na mtu binafsi tumempa dakika tano," alisema.

**KAULI YA ACT**

Wakati CHADEMA wakiyasema hayo, Chama cha ACT-Wazalendo kimesema licha ya serikali kupeleka bungeni miswada hiyo na vyama siasa kuanza kuchukua maoni mbalimbali ya wadau, kinaona miswada hiyo haijagusa maeneo muhimu ili kuimarisha demokrasia.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Waziri Mkuu Kivuli wa chama hicho, Doroth Semu, alisema mazingira hayo ya kukosekana maeneo muhimu ya kuimarisha demokrasia yatasukuma chama hicho kupigania zaidi uwanja huru wa kufanya siasa za kidemokrasia.

"Ingawa serikali imechukua hatua hiyo, bado miswada hii haijagusa maeneo muhimu ili kuimarisha demokrasia," alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa kuna maandalizi ya uchaguzi wa wenyeviti na wajumbe wa serikali za mtaa kwa Tanzania Bara na chama hicho kimeendelea kusisitiza uchaguzi huo usisimamiwe na TAMISEMI na badala yake usimamiwe na Tume Huru ya Uchaguzi.

Kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo pia alitaka serikali ichukue hatua dhidi ya migogoro ya ardhi na ubadhirifu wa fedha za umma.

Doroth pia alizungumzia kukua kwa Deni la Taifa, akisema ACT inaendelea kuitaka serikali ipunguze uwiano wa mikopo ya kibiashara kwenye Deni la Serikali hadi kufikia asilimia 20 ifikapo mwaka 2025, ambao ni ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

# Onyo la Waziri Mkenda lapokewa kwa shangwe

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI wazazi wakipongeza uamuzi wa serikali wa kupiga marufuku shule binafsi kuwakataa wanafunzi walioshindwa kufikia alama za ufaulu katika shule zao, Shirikisho la Wamiliki wa Shule na Vyuo Binafsi nchini (TAMONGSCO) limeshangaa jambo hilo kuendelea shuleni.

Juzi, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, wakati akizungumzia matokeo ya Upimaji wa Taifa wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili, alionya shule ambazo zina tabia ya kuwaondoa wanafunzi ambao hawajafanya vizuri.

Baadhi ya wazazi waliiambia Nipashe jana kuwa kuna shule zimekuwa na tabia hiyo ambayo huwaumiza na watoto wao.

Mzazi Japhet Kabelega aliipongeza serikali kwa kuendelea kuingilia kati na kukemea shule zinazochuja watoto kwa kutofikisha wastani walioweka hata kama mtoto amefikia wastani wa serikali, kwa kuwa hali hiyo inawarudisha nyuma wazazi kimaendeleo.

Kabelega alisema alijikuta akiingia gharama kubwa ya kuhamisha mtoto wake baada ya shule aliyokuwa akisoma awali, kumkataa kwa kushindwa kufikisha wastani walioutaka licha ya kuvuka wastani uliowekwa na serikali.

Alisema hakuona haja ya shule hiyo kuchukua uamuzi huo, bali wangefanya utaratibu wa kumsaidia mtoto ili aongeze uelewa, huku akiendelea na masomo yake ya darasa la tano.

Mdau wa elimu, Maria Fwaisa, aliunga mkono maagizo ya waziri huyo, akisisitiza shule hizo kujikita katika kuinua taaluma kwa watoto na si kuchagua wale waliozaliwa na uelewa wa juu.

"Kwa hiyo ninafikiri suala hilo liendelee kupigiwa kelele ili kila mtoto nchini apate haki ya elimu bila kujali hali yake, lakini pia mzazi wake asibughudhiwe, lengo liwe ni kukuza taaluma na si kuchagua wenye uelewa wa juu ili shule ipate alama A," alisema.

Mwenyekiti wa TAMONGSCO, Leonard Mao, alisema serikali imekuwa inakemea suala hilo mara kwa mara na hivyo anasikitishwa kusikia bado kuna shule zinawakataa watoto waliopata alama za chini katika mitihani hiyo.

Alisema jambo hilo siyo sahihi kwa kuwa lengo la kuwapokea watoto hao ni kuwakuza kitaaluma na kuzisihi shule zinazofanya hivyo kuacha mara moja kwa kuwa inaweza kuua sifa ya shule.

Alisema katika vikao vyao wamekubaliana ikiwa mwanafunzi atafikia viwango vilivyowekwa na serikali, lakini hakufikia vya shule husika, anapaswa kuendelea na madarasa ya juu, huku akipatiwa msaada wa ziada ili kufikia viwango vya shule.

"Mzazi ambaye mwanawe amefikia viwango vya serikali na shule ikataka arudie darasa au ikamkataa, mzazi ana haki ya kwenda kushtaki katika mamlaka za serikali kwa kuwa anapaswa kuendelea na shule huku akipatiwa masomo ya ziada ili afikie viwango vya shule," alisema.




NANGE AUCTIONMART AND DEBT COLLECTORS LTD
MANYARA BRANCH
AUCTIONEERS, DEBT COLLECTORS COURT BROKERS, PROPERTY VALUERS AND COMMISSION AGENTS

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na Mashati saccos kampuni ya Nange Auction Mart itauza kwa mnada wa hadhara mali za wadiwa walioshindwa kulipa madeni yao

| S/N | JINA | DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | FELIX TEMU | SHAMBA | ROMBO-MASHATI | 23/1/2024 saa 5:00 asubuhi Nakuendelea |
| 2 | VICTUS MARANDU | SHAMBA | ROMBO MASHATI | 24/1/2024 saa 4:00 asubuhi Nakuendelea |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa katika mnada, salio litalipwa ndani ya siku 14 toka tarehe yam nada huu. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mnada wa siku 14 atakuwa amepoteza haki yake mnada utarudiwa na 25% aliyolipa haitarudishwa
2. Wateja wataruhusiwa kukagua mali husika kabla ya mnada **: Mawasiliano 0766538295**



MASTERMIND
TOBACCO TANZANIA LTD

## JOB ANNOUNCEMENT

**1. Tobacco Primary Manufacturing Department (PMD) Manager;**

**Job Summary:** PMD Manager reporting to the General Manager, is responsible for ensuring daily factory/ tobacco operations are within the approved standards, overseeing / recording cigarette manufacturing and maintaining supporting documents while assisting the General Manager in his daily functions.

**Job Summary:**

**Job Description**
- Ensure the correct implementation of production processes in a safe environment for the team based on IWS.
- Ensure product compliance with quality standards.
- Ensure the accurate implementation of the production plan.
- People management (vacation, performance evaluation, hiring, promotion, etc.).
- Hold shift meetings in the production line to eliminate waste and increase efficiency.
- Ensure the exact implementation of the rebranding process.
- Follow up on production problems and operator/technician support when needed.
- Prepare production shift reports.
- Compare performance results with established standards, identifying deviations, trends, or abnormal changes and their causes.
- Ensure that the required production in the cell is manufactured in the required time, within the laid down specifications and at the lowest cost, thus ensuring the utilization of all resources to the optimum.
- Responsible for department administration and the utilization of Human Resources.

**Requirements**
- At least 5 years of work experience as a production supervisor (work experience in the tobacco processing industry is an advantage).
- Bachelor's degree in Mechanical Engineering, Chemical Engineering, or Industrial Engineering.
- Familiar with Integrated Work System (IWS) and production processes.
- Ability to work in shifts.
- Ability to manage people.
- Strong and effective communication.
- Responsible for production personnel and having a teamwork spirit.
- The appropriate speed of action for solving production line problems, reducing interruptions in production, increasing the efficiency of devices, and reducing production waste.
- Ability to prepare relevant reports from work shifts.
- Perform all other duties as and when assigned by the management.
- Any other related factory accomplishment tasked by the General Manager, Head office and Directors.

**Skills:**
- Think/Operate strategically
- Decision making
- Make Things Happen
- Lead/Manage Change
- Motivate/Develop people
- Teamwork skills
- Communication and interpersonal skills
- Personal responsibility for development
- Problem solving skills
- Computer literacy
- Financial skills.

**2. Senior Accountant**

**Job Summary:** Senior Accountant reporting to the General Manager, is responsible for ensuring daily transactions are within the approved budget, approval of payment vouchers, overseeing / recording transactions and maintaining supporting documents while assisting the General Manager in his daily functions.

**Job Description**
- Receiving payment requests from the business functions.
- Ensuring the payment requests are within the approved budget. If not within the approved budget, request for approval through the General Manager.
- Invoicing to local and export customers and ensuring all payment are supported by legitimate source documents.
- Monitor and control cash floats maintained with the Cashier(s).
- Ensuring to fill and record all Payment Vouchers in TALLY system on a timely manner.
- Preparation of weekly and Monthly management Cash Flow and submission to the General Manager.
- Maintenance of Creditors and Debtors records.
- Preparation of Bank reconciliations and liaising with banks to obtain statements.
- Monitoring bank charges and exchange losses as applicable.
- Inventory management and stock reconciliation at different production levels.
- Working closely with other departments in order to control costs.
- Preparation of any other ad-hoc reports as requested by the General Manager
- Assisting the General Manager in preparation and filing of annual Financial Statements in liaison with the external auditors.
- Ensure direct and indirect tax compliances, assisting in periodical government controls/audits carried out by various Government organizations.
- Maintain relationships with banks, Government Authorities, statutory auditors, tax advisors.
- Perform all other duties as and when assigned by the management.

**Requirements;**
- Degree in Finance or accountancy, or relevant field
- Professional Accounting – Registered CPA by NBAA Tanzania
- At least 6 – 8 years of experience in a similar position / function.
- Preference to experience within the agriculture industry.
- Computer Knowledge: Good knowledge of MS excels and computer accounting software, such as SAP/TALLY and other relevant ERP accounting software.
- Demonstrated excellent organizational, coordinating, and personal interface skills.
- Proven job diligence, dedication, and attention to detail.
- Commitment to work overtime on occasions and when required.

**Skills:**
- Think/Operate strategically
- Decision making
- Make Things Happen
- Lead/Manage Change
- Motivate/Develop people
- Teamwork skills
- Communication and interpersonal skills
- Personal responsibility for development
- Problem solving skills
- Computer literacy
- Financial skills.

**All applications shall be addressed online to**
**Human Resources Manager**
**Email: info@mtt.co.tz**
**Deadline shall be 22nd January 2024.**

RIPOTI MAALUM

## MJAMZITO ALIYEBAKWA

# Avimba tumbo, miguu, hatembei, ana vidonda

## -Waziri ang'aka, aagiza wahusika wakamatwe

Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa
MKURANGA

MJAMZITO aliyebakwa wilayani Mkuranga, mkoani Pwani miezi minane iliyopita, amepata madhara kiafya na sasa anakabiliwa na orodha ya matatizo yanayohitaji tiba:

Miguu yake imevimba, imepasuka na kunashuhudiwa vidonda; mzunguko wa siku zake za hedhi umeongezeka zaidi, huku tumbo lake likijaa na dokezo la awali la matabibu ni kwamba "limejaa gesi".

Haja kubwa ambayo ni sehemu ya uhalisia wa binadamu, kwake inachukua hata siku nne bila kuipata; hana uwezo wa kutembea, haja zote analazimika kuzimaliza ndani.

Katika maisha ya kawaida hana wa kumhudumia. Kwa jicho pana, muwewe aliyepaswa kuwa msaada, ni dereva bodaboda, anahangaikia ajira yake ili kuwawezesha mkewe na watoto wao wawili maisha yaende.

Juni 5, mwaka huu, mama huyo mkazi wa Mtaa wa Kazole, Kata ya Vikindu, wilayani Mkuranga, alibakwa na hatimaye kufungwa katika kiroba.

Wiki sita baadaye, ujauzito wake uliothibitika hospitalini kuwa wa pacha uliharibika. Akajifungulia Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga watoto wawili - si riziki - Julai 12, mwaka huu.

Jumapili iliyopita, mwandishi wa habari hizi, alifika nyumbani kwa mama huyo na kubaini shida mpya zinazomkabili kiafya, ikiwa imepita miezi minane pasi na Jeshi la Polisi kuchukua hatua dhidi ya waliotenda ukatili huo.

Hapo ndipo mwandishi alipomtafuta kwa simu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ambaye baada ya kusimuliwa mkasa mzima, aliagiza watendaji walio chini yake kuanzia ngazi ya wilaya hadi wizarani wachukue hatua za dharura kuhakikisha mama huyo anapatiwa matibabu.

Mume wa mwathirika wa ukatili huo (jina tunalihifadhi), alimwambia mwandishi jana kuwa Jumapili jioni, Mwenyekiti wa Mtaa wa Kazole, Kazbert Mwaya, alifika nyumbani kwake kumchukua mkewe na kumpeleka Kituo cha Afya Ngunguti kilichoko Kata ya Vikindu.

"Alisema alipigiwa simu na mamlaka za juu, akaagizwa kumpeleka hospitalini kwa ajili ya matibabu. Tukiwa (Kituo cha Afya) Ngunguti, mke wangu alisafishwa vidonda vya miguuni, baada ya muda kidogo alikuja Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya akatupakia kwenye gari lake, akatupeleka Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga.

"Kuna karatasi tulipewa Ngunguti, tulipofika Hospitali ya Wilaya, daktari alichukua kisha mke wangu akalazwa wodini, akatundikiwa dripu za maji, alipatiwa dripu nne siku hiyo ya Jumapili.

"Asubuhi siku iliyofuata (Jumatatu) alifanyiwa vipimo vya x-ray na utrasound. Baadaye daktari alituambia wamebaini kuna shida tumboni ambayo imeathiri hata utumbo.

"Tuliruhusiwa kutoka hospitalini jana (Jumanne) jioni baada ya mke wangu kupata nafuu. Tulipewa dawa (vidonge) na vifaa vya kusafishia vidonda vinavyomsumbua. Gharama za matibabu zimebebwa na serikali," alisema huku akimshukuru mwandishi kwa kulifikisha suala hilo wizarani.



Hali ya mwathirika huyo ilivyokuwa Jumapili iliyopita.

Mkewe (jina tunalihifadhi), katika mazungumzo na mwandishi Jumapili nyumbani kwake Mtaa wa Kazole, alisema: "Hali yangu kiafya kama unavyoona si nzuri, siwezi hata kutembea, miguu imevimba na inapasuka na kuota vidonda, ninajisaidia haja zote humu ndani. Tumbo limevimba sana na sipati hamu ya kula kabisa.

"Tangu wale watoto wangu pacha walipofia tumboni, mwili wangu hauko vizuri kiafya, mwili mzima unauma, mikono, miguu inauma. Kwa kweli ninapata tabu sana!

"Kuanzia mwezi wa 10 (Oktoba) mwaka jana, ninaona siku zangu mara tatu kwa mwezi. Kutembea kwa sasa siwezi. 'Kila kitu' ninafanya hapohapo ninapokaa."

Ofisa katika Idara ya Ustawi wa Jamii wilayani Mkuranga, Lillian Kokwakila, ndiye aliyekwenda Kituo cha Afya Ngunguti Jumapili na kumchukua mgonjwa huyo. Anasema alifanya hivyo kwa maelekezo ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Hadija Nasri Ali.

**KAULI YA WAZIRI**

Baada ya mama huyo kupatiwa matibabu na kuruhusiwa kutoka hospitalini Mkuranga juzi, Waziri Dorothy alitoa kauli rasmi kuhusu tukio hilo, akiagiza Jeshi la Polisi kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya wahusika wa ukatili huo.

Alisema ukatili huo ni matokeo ya anguko la malezi ngazi ya familia ambako mtoto hutakiwa kulelewa na kuwekewa misingi ya utu mwema, hofu ya Mungu na uadilifu.

"Hivyo, wazazi na walezi kila mmoja atimize wajibu wake. Mzazi au mlezi na jamii akibaini mtoto mtukutu asiyeshika maadili, ni vyema kutoa taarifa mapema Ili apelekwe kwenye vyuo vya ustawi wa jamii vya marekebisho ya tabia kwa watoto wakiwa bado wadogo.

"Ukatili si utu na si ucha Mungu na ni kinyume cha sheria. Hivyo, waliofanya ukatili huu na wengine kama hawa, tutafuatilia kuhakikisha sheria inachukua mkondo wake.

"Jamii yote inatakiwa kuwekeza kwenye malezi na makuzi ya watoto na pia kuungana kupiga vita ukatili wa aina yoyote kwani hakuna aliye salama iwapo kwenye jamii kuna watu katili.

"Jamii ya sasa imeelimika sana na iko vitani dhidi ya ukatili. Hivyo, hakuna katili atakayekwepa mkono wa sheria. Jamii itoe taarifa na serikali itafuatilia kikamilifu na haki itatendeka kwa waliofanya ukatili huu na kwa wengine wote," Dk. Dorothy alisema.



Dk. Dorothy Gwajima.

# Mikopo boti za uvuvi yazinduliwa Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amezindua huduma ya mikopo nafuu ya boti za kisasa za uvuvi na vifaa vyake inayotolewa na Benki ya NMB, akitaja taasisi hiyo kuwa msaidizi mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika kukuza uchumi wa buluu na kuwaletea maendeleo endelevu wananchi.

Katika viwanja vya Skuli ya Msingi Tasini iliyoko Kiwani, Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed aliipongeza benki hiyo juzi alipozindua mikopo hiyo na kupokea boti tano za mkopo na vifaa vyake, zikiwa zimekatiwa bima, zikitolewa na benki hiyo kwa Jumuiya ya Wavuvi Kiwani (Juwaki).

Sambamba na uzinduzi na makabidhiano ya boti hizo, Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi wa NMB, Filbert Mponzi, alimkabidhi Makamu wa Rais msaada wa vifaa vya kuezekea vyumba vya madarasa ya skuli tatu za Chambani, Pondeani na Nanguji, zilizoko Kiwani, ambavyo ni mabati 400, mbao na misumari, vyenye thamani ya Sh. milioni 22.

Makamu wa Rais Hemed aliipongeza NMB kwa kusikiliza maombi ya wananchi wa Kiwani na kuyafanyia kazi kwa haraka, huku akibainisha kwamba boti za kisasa ilizokabidhi kwa Juwaki, zinaakisi na kusaidia dhamira na Sera ya Uchumi wa Bluu inayotekelezwa na SMZ chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

"NMB imejipambanua kuwa ni moja ya benki kubwa Afrika na SMZ inajivunia ushirikiano uliopo baina yetu na taasisi hii, ambayo imetusaidia sana katika maeneo mbalimbali.

"Tunaishukuru sana kwa namna inavyowatendea haki Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla, kwa sababu kila eneo, kila sekta serikali ilikopiga hatua, benki hii imekuwa nyuma yetu.

"Leo (juzi) wamekuja hapa kutimiza maombi yetu wana Kiwani ambayo niliyatoa kwao ya kutukopesha vifaa vya kisasa vya uvuvi, kwani serikali yetu inataka kuwafanya wananchi wa hapa wanakuwa 'busy' kwa shughuli za kimaendeleo.

"Boti hizi tano zinakwenda kuwaweka 'busy' wavuni 20, ambao nyuma yao kuna mnyororo mpana wa wasaidizi wa shughuli zao," alibainisha.

Aliwataka Juwaki kuhakikisha wanazitumia vyema boti hizo kwa kurejesha kwa wakati ili kutoa fursa ya wakopaji wengine kufikiwa na huduma hiyo, na kuwataka kutojiuliza soko la bidhaa za uvuvi, kwa kuwa hilo ni jukumu la serikali ambayo inapambana kuweka mazingira bora, huku akiwaahidi kuwanunulia mafuta ya kuanzia kazi kwa boti zote (lita 30 kila moja).

"Ninaamini hamtoniangusha na hapa niwahakikishie NMB, kwamba Juwaki na wanachama wao wameniahidi kuwa watalipa marejesho ya mikopo hii kwa kasi kubwa na watamaliza kabla ya muda watakaopangiwa, na mimi ninawaahidi kwamba nitawasimamia," alisema Makamu wa Rais.

Mponzi aliipongeza Serikali ya Awamu ya Nane chini ya Rais Dk. Mwinyi kwa mchakato endelevu wa uchumi wa buluu, huku akibainisha kuwa siri ya ushirikiano mkubwa uliopo baina ya NMB na SMZ ni uzuri, ubora na umuhimu wa maono, mipango na malengo ya serikali hiyo, yanayowasukuma kuguswa nayo na kupambana kuyasaidia utimilifu wake.

"SMZ ilituonesha ilivyo na mipango ya kuvutia na kimsingi imefanya makubwa hadi sasa. Na sisi tunatumia fursa hiyo kuisapoti na kutokana na mazingira wezeshi iliyoyaweka, imetuwezesha kutanua mtandao wetu wa matawi Zanzibar na Pemba, huku tukijiandaa kufungua tawi jipya Wete, hapa Pemba, lengo ni kufikisha huduma kwa jamii na kuharakisha maendeleo yao.

"Hapa tunakabidhi boti tano zenye nyavu na vifaa vya usalama (maboya na bima), kupitia 'NMB MastaBoti' ambayo imekuja kuwawezesha wavuvi wa kada zote ambao tunajitoa kuboresha mazingira yao ya utendaji kazi. Huu ni mwanzo, kadri watakavyolipa kwa haraka, ndivyo tutavyowafikia wavuvi wengi zaidi," alisema Mponzi.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali, wakiwamo Waziri wa Uchumi wa Buluu, Suleiman Masoud, Waziri wa Maji na Nishati, Shabib Hassan Kaduara, Mkuu wa Wilaya ya Mkoani, Khatib Juma Mjaja, Mbunge wa Kiwani, Rashid Abdallah Rashid, Mkuu wa Biashara NMB Zanzibar, Naima Shaame na Mkuu wa Idara ya Kilimo NMB, Nsolo Mlozi.

# Kiswahili kutumika rasmi Afrika Mashariki

**Na Christina Mwakangale**

BARAZA la Kiswahili la Taifa (BAKITA), limetoa wito kwa Watanzania waliobobea katika lugha ya Kiswahili, hususan wakalimani, kuchangamkia fursa ya soko la ajira lililopo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambayo mwaka huu inaanza kutumika rasmi EAC.

Kauli ya BAKITA, imekuja baada ya Januari 9, mwaka huu, Katibu Mkuu wa EAC, Dk. Peter Mathuki, alipofanyiwa mahojiano na Idhaa ya Kiswahili Umoja wa Mataifa, alisema utekelezaji unaanza rasmi.

"Imepitishwa na inafungu la kuwezesha lugha tatu kutumika ambazo ni Kingereza, Kifaransa na Kiswahili, bajeti yetu ya mwaka huu, tumeweka mikakati yote kuwa na watafsiri wa makabrasha yote.

"Tuwaajiri wataalamu wa Kiswahili, pia kwa lugha ya Kiingereza, Kiswahili na Kifaransa," alisema Dk Mathuki.

Akifafanua kuhusu suala hilo, Katibu Mtendaji BAKITA, Consolata Mushi alipozungumza na Nipashe, jana, alisema kwa kauli hiyo ni kwamba utekelezaji unaanza rasmi, licha ya awali kufahamika lugha hiyo imekwishatolewa taarifa ya kutumika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Ni fursa kwa wakalimani wetu kwenye soko hili la EAC, pamoja na kwamba tayari ulikwishafanya kazi ya ukalimani na EAC, ila haikuwa rasmi sana, kwa tamko hilo ni kwamba utekelezaji utaanza 2024," alisema Consolata.

Kiswahili kilitangazwa rasmi kutambuliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni (UNESCO) na kila mwaka Julai 7, dunia inaadhimisha siku hiyo.

Katibu Mkuu alisema EAC ina takribani watu milioni 350 inaitegemea lugha hiyo kutoka nchi wanachama Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC) na Somalia.

"Kiswahili tunakitegemea sana sababu wananchi wengi katika jumuiya yetu wanaelewa lugha ya Kiswahili kwahiyo hii sasa itakuwa kazi yetu sisi kama watendaji wa jumuiya kuhakikisha kwamba habari zote na vikao vyote vinafanyika kwa lugha ya Kiswahili."

"Hakikuanza rasmi kutumika, shida ilikuwa ni Kiswahili hakikuwapo kwenye Katiba ya jumuiya, lakini sasa baada ya kusema turekebishe katiba ya jumuiya na kuweka lugha hiyo si tu bungeni bali kwenye vikao vyote vya jumuiya na hiyo sasa tumeanza mikakati yake," alisema Dk. Mathuki.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa shule shikizi (awali) ya kijiji cha Kamguruki, Musoma Vijijini mkoani Mara juzi, ili kupunguzia watoto wadogo kutembea umbali mrefu kufuata elimu.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yaja na mkopo wa ada kukabili ugumu wa Januari

**Na Joseph Mwendapole**

KATIKA kuwasaidia wazazi kupunguza makali ya mwezi Januari, Benki ya Mwanga Hakika imezindua huduma ya mkopo wa ada kwa wazazi kuwasaidia kufanikisha kulipia karo za wanafunzi kwa urahisi.

Imezoeleka mwezi Januari kutajwa kuwa kuwa "mwezi mgumu" kutokana na kuwa kipindi cha majukumu mengi kwa watu wengi, huku hali ya kiuchumi kwa wengi ikiwa si rafiki kutokana na matumizi ya kipindi cha mwisho wa mwaka.

Benki ya Mwanga Hakika kwa kuliona hilo, imeamua kuwasaidia wazazi kufanikisha malengo ya kielimu kwa watoto wao kwa kulipa ada kwa wakati na kwa urahisi kupitia mkopo wa ada unaotolewa ndani ya saa 24.

Wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo juzi, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo na Kati wa benki hiyo, Mwinyimkuu Ngalima, alisema wamekuwa mstari wa mbele kuleta suluhu ambazo zinawasaidia wateja kufanikisha malengo mbalimbali kwa urahisi zaidi ili kuboresha maisha yao.

Alisema benki hiyo inatambua umuhimu wa elimu na ndio maana imekuja na huduma ambayo inalenga kuwasaidia wazazi kuweza kulipa karo za wanafunzi na kupunguza adha wanazokumbana nazo kipindi hiki cha mwanzo wa mwaka.

"Tunatambua kwamba elimu ni haki ya msingi kwa kila mtoto na ndio maana tumekuja na huduma hii ya mkopo wa ada kwa wanafunzi ili kuwapunguzia wazazi mzigo na hatimaye kila mwanafunzi aweze kwenda shuleni," alisema.

Ofisa huyo wa benki alisema hatua hiyo pia imelenga kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu nchini.

"Huduma hii inapatikana kwa wazazi, walezi na wadhamini wa wanafunzi kwa shule zote za msingi na sekondari ambazo zina makubaliano (MoU) na Mwanga Hakika Bank.

"Uombaji wa mkopo huu ni rahisi na ni nyaraka chache zinazohitajika kukamilisha mchakato wake," alisema.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ugonjwa wa kipindupindu usichukuliwe poa

**HABARI** za kuripotiwa ugonjwa wa kipindupindu kutoka katika mikoa mbalimbali na kusababisha vifo ni lazima zichukuliwe kwa umakini ili kudhibiti ugonjwa huo usisambae zaidi nchini.

Tayari nchi jirani ya Zambia imeripotiwa ugonjwa huo kuua na kuambukiza wengine kadhaa.

Mwingiliano wa watu kutoka nchi moja kwenda nyingine kwa milipuko ya magonjwa haya husababisha kusambaa kwa kasi na kuleta taharuki kubwa.

Suala la usafi ni muhimu katika kudhibiti ugonjwa huo ambao kwa asilimia kubwa husababishwa na uchafu.

Kipindi hiki cha mvua inayoendelea kunyesha magonjwa ya milipuko ikiwamo ya matumbo na kuhara ndio huibuka kwa kasi.

Wakati ugonjwa wa Uviko-19 ulipotikisa dunia, ugonjwa wa kipindupindu ulipotea kabisa nchini kwa sababu watu walikuwa wanazingatia usafi hasa wa kunawa mikono kwa sabuni kila wakati.

Watu walijijengea utaratibu wa kunawa mikono kila wanapotoka kushika vitu kwenye mijumuiko ya watu au kushika vitakasa mikono ambao ulisaidia sana kuepuka ugonjwa wa kipindupindu kwa sababu hapo awali walikuwa na uthubutu wa kununua matunda au chakula na kula bila hata kunawa au kushikana mikono bila kujali mtu huyo ametoka wapi na ameshika nini kwa wakati huo.

Hapa nchini mikoa ambayo tayari ugonjwa huo umesharipotiwa ni Mwanza ambapo Mkuu wa Wilaya ya Magu, Rahel Kasanda amethibitisha kutokea kwa kifo cha mtu mmoja aliyethibitika kuwa na ugonjwa wa kipindupindu huku wenzake 20 wakiambukizwa.

Inadaiwa alikutwa na ugonjwa huo baada ya kutoka kwenye sherehe ya mmoja wa wake zake iliyofanyika Dutwa mkoani Simiyu.

Kipindi hiki cha milipuko ya ugonjwa wa kuambukiza si kizuri kwa watu kujumuika katika sherehe kwa sababu maambukizo husambaa kwa kasi kubwa sana.

Watu wajaribu kujiepusha kwenda kwenye mchanganyiko wa watu wengi ili kujiweka salama na kuepukana na ugonjwa huo.

Pia, imethibitika kuwa watu walioshiriki katika msiba wa mtu huo ndio wagonjwa waliokutwa na ugonjwa huo na kukimbizwa kupatiwa huduma za afya na kati yao saba waliruhusiwa huku wengine 13 wakiendelea kupatiwa matibabu.

Mganga Mkuu wa Jiji la Mwanza, Sebastian Pima, alithibitisha kupokea wagonjwa wawili kwenye Kituo cha Afya Igoma walitokea katika msiba huo na baada ya vipimo walibaini kuwa na maambukizi ya kipindupindu.

Kipindupindu ni ugonjwa wa aibu kwa sababu unatokana na uchafu, hivyo ni muhimu kila mtu ajitahidi kujiepusha kuupata kwa kuzingatia kanuni za usafi.

Kanuni na taratibu za afya ni pamoja na kunawa mikono kwa maji tiririka kabla na baada ya kula kwa kuwa vimelea hao wa ugonjwa huingia mwilini kupitia kula vitu vichafu.

Kadhalika watu waache kula vyakula vilivyopoa kwa sababu vimelea wa ugonjwa huu wa kipindipindu wanaishi katika mazingira ya vyakula vya baridi pia watu wachemshe au kuyatibu maji ya kunywa ili kuwaua wadudu hao wasiingie mwilini.

Ni vizuri pia viongozi na wananchi wakashirikiana katika kutoa elimu mara kwa mara ili kukumbushana umuhimu wa kuweka mazingira safi kuepukana na vimelea vya ugonjwa huo.

Wananchi pia waache tabia ya kununua vyakula katika maeneo hatarishi na wanaopika vyakula vinavyouzwa mitaani wazingatie usafi wa vyombo wanavyotumia kutayarishia vyakula hivyo na mazingira wanayopikia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# TRC mjue kumfutia ruti Chalamila, treni ya Mwakyembe, mnamkaidi ...

**NAOMBA** niongee kama mwanasiasa. Kwanza enyi TRC, kwa niaba yenu na kwa niaba yetu sisi abiria, tumshukuru sana msomi, Dk. Harrison Mwakyembe, kubuni usafiri wa 'daladala' ya treni, mtu anatoka Kariakoo na kufika Pugu chini ya dakika 50.

Achana na sisi abiria tunaopata nafuu, nikiwaangalia 'ma-titi' walivyo bize kukatisha tiketi, si haba, kipengele cha mshahara kuchelewa kwenu ni ukorofi wa mhasibu au bosi mwingine.

Sasa sisi tulivyofundishwa utotoni, ukinunuliwa viatu au kaptura, awe mjomba au baba mwenyewe, mbali na ahsante, dhamana inayotubakia ni kuitunza hiyo.

Hapo na nyinyi mtunze hivyo mlivyoanzishiwa na mjomba Mwakyembe. Nakumbuka miezi miwili tu iliyopita, mlifanya 'madudu' hapo, abiria kudandia mpaka kwenye kichwa, Mama Mkuu wa Nchi, akamkurupua Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila. Nimsifu akawa mjeshi kweli kweli, akawakurupueni menejimenti ya TRC kwa ukaguzi wa mambo kibao, yakapatikana makosa 10 na ushehe.

Hata mwenyewe Chalamila, hakuwakopa, akawaeleza kakurupushwa, akawaagiza cha kufanya kurekebisha hizo shida. Leo hii miezi miwili tu, mmerudi pale pale.

Kwangu mimi maana yake 'mnampotezea' Mkuu wa mkoa, lakini baya zaidi mmevamia pori la miba, maana lile ni la Mama. Nini mnakitafuata? Mimi sijui, ila ukweli unabaki, moyo unadunda ile mbaya.

Ni juzi tu, nimeshuhudia abiria wa saa 4:30 usiku Kariakoo wanaoondoshwa saa 7:00 usiku kwenda Pugu, tena baada ya vurugu kwenye ofisi zenu, mhusika wake anapotea, anamuachia magumu mwenye nyota kadhaa begani. Kwani yeye ndiye ofisa ya TRC? Hapo hapo kwanza tuweke nukta, hivi neno kuwajibika lina maana gani kwenu?

Wakati bado tunashangaa mazito ya Jumatatu, juzi usiku, masikini abiria wa watu wa saa nne usiku, wamechoka ile mbaya, watumishi wenu pale getini wakawajibu kilaini tu, 'katafuteni kwingine, leo treni hamna.' Wakati tripu hiyo ya usiku ni agizo la Rais kupitia kwa Mkuu wa Mkoa. Jamani makubwa, mbona madogo yana nafuu!

Wengi tunajiuliza, kwanini sikuhizi mambo yenu yanaenda shaghalabagala wakati huko nyuma usafiri wa 'daladala' za treni ulikuwa ndiyo kama mkombozi kwa wakazio wa ruti ya Pugu?

Kwa nini usafiri umekuwa na shida kiasi cha kuzusha msongamano mkubwa wa abiria ambao umekua na athari kuwa kwa wasafiri hao wakiwemo wanawake na watoto, hasa wanafunzi. Si bure kuna namna!

Sasa mbona alipokuja Mkuu wa Mkoa, menejimenti wa TRC hamkuwasilisha matatizo yenu ili mamlaka husika iweze kuwawezesha ili muendelee na huduma kama kawaida.

Kwa nini hamkumwambia kuna tatizo au changamoto la miundombinu, mabehewa machache, injini mbovu au mengine ambayo yanasababisha usafiri uwe wa shida?

Mwenyewe mkuu wa mkoa alipokuja hapo na kufanya ukaguzi wake Novemba 9 lilipotokea tatizo linalofanana na hili, akiwakusanya mabosi kibao alibainisha kasoro nyingi ambazo treni kutozingatia ratiba, kutotolewa risiti, abiria kutorejeshewa fedha, hakuna sehemu ya kujisitiri mvua, vyoo, nidhamu mbaya na uonevu wa polisi, mabehewa machache ya wanafunzi na idadi chache ya safari.

Nia yangu hapa siyo kutaka kuwahukumu moja kwa moja menejimenti ya TRC, lakini kama kuna matatizo kwa nini hamyasemi? Na kama hamruhusiwi kuyasema kwa nini hamuonekani kutatua?

Imefika wakati sasa menejimenti ya TRC hata kama haitotoka na kuwaomba radhi abiria, lakini ikae na kujifungia ndani ili kuangalia tatizo liko wapi na wao wanaweza kufanya nini ili kupunguza au kumaliza tatizo hilo.

Huo ndiyo ukubwa, vyeo walivyonavyo, mishahara siyo kwa ajili ya kukaa ofisini tu, bali ni kuangalia pia changamoto na jinsi ya kuyatatua.

Pia wakati mwingine viongozi wajifunze kuwa hata kama mambo yatakuwa yanakwenda vizuri, lakini wawe na muda wa kukaa na kuangalia kama tatizo likitokea ghafla la usafiri watalikabili vipi. Huu ndiyo uongozi. Fanyeni hivyo.

HABARI KITAIFA

## Shule binafsi zaongoza usajili mafunzo ya amali

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda, amesema shule binafsi zinaongoza kwa kuwa na mwitikio mzuri wa kusajiliwa kufundisha mafunzo ya amali ambayo yataanza kutolewa rasmi katika shule za sekondari.

Amesema kwa sasa katika shule za sekondari kutakuwa na mikondo miwili, ukiwamo wa mafunzo ya amali ambao utatoa elimu sawa na inayotolewa kwenye vyuo vya ufundi na elimu jumla itakayotoa mafunzo ya sekondari ambayo pia yamepunguzwa kutokana na mtaala mpya.

Prof. Mkenda aliyabainisha hayo jana mkoani Dodoma, akieleza kuwa shule zitapata idhini ya kufundisha mafunzo ya amali endapo itathibitishwa kuwa na vifaa vya kutosha na walimu.

"Kwa mwaka huu kuna shule 28 za serikali, na 68 za binafsi, ndizo zimepata idhini ya kutoa mafunzo ya amali kwa michepuo mbalimbali, hivyo hatutaruhusu shule ianze kutoa mafunzo hayo bila kuwa na vifaa stahiki.

"Kwa mfano, kama shule inataka kufundisha mapishi lazima tuone kuna jiko na vitu ambavyo vinaweza vikamsaidia mwanafunzi kupata uelewa unaotakiwa na ninashukuru shule ambazo si za serikali zimeenda kwa kasi kuliko hata zile zinazomilikiwa na TAMISEMI," alisema.

Alisema serikali imeweka miongozo ya namna ya kuwekeza kwenye miundombinu ya shule ili watoe elimu jumuishi na wanafundisha walimu wengi zaidi ambao wanaweza kumudu kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu.

Vilevile, alibainisha kuwa kwa sasa serikali inatoa vitabu vyote vyenye maandishi yaliyokuzwa na ya nukta nundu kuanzia elimu ya awali mpaka kidato cha sita pamoja na viti mwendo kwa ajili ya wanafunzi ambao wana changamoto ya kutembea.

"Kwa wale wenye changamoto kubwa zaidi tunawapeleka shule maalum ya Patandi, Arusha na Lukuledi ya Masasi, mkoani Mtwara ili kuwapa huduma vizuri zaidi," alisema Prof. Mkenda.




Mkuu wa Idara ya Wateja Wadogo na Kati wa Benki ya Mwanga Hakika, Mwinyimkuu Ngalima (katikati), Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wakubwa, Projest Massawe (kushoto) na Meneja Mwandamizi wa Wateja Wadogo na Kati, Hamisi Chimwaga, wakizindua huduma ya mkopo wa ada usio na dhamana unaotolewa ndani ya saa 24 kwa wazazi, walezi na wadhamini wa wanafunzi jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Diwani, wenzake wanne mbaroni tuhuma kuuza shamba la serikali

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

VIONGOZI watano wa Kata ya Iborogero, wilayani Igunga mkoani Tabora akiwamo diwani wa kata hiyo, Emmanuel Bundara (CCM) wanashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Igunga kwa tuhuma za kuuza mashamba ya Wizara ya Mifugo yaliyotengwa na serikali kwa ajili ya kufanyia shughuli za wanyamakazi.

Akithibitisha tukio hilo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Iborogero, Robert Mwagara, alisema lilitokea Januari 4, mwaka huu na kuwataja wanaoshikiliwa kuwa ni Kaimu Mwenyekiti wa Kijiji cha Iborogelo, Khalifa Juma, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Iteleleja, Deo George, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mwankolo, Shija Budohya na Mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Iborogelo, Seif Maulidi.

Aidha, Ofisa Mtendaji huyo alibainisha kuwa maofisa hao wa TAKUKURU walifika katika ofisi za kata hiyo Januari 4, mwaka huu saa 11 jioni waliongozana hadi kwenye eneo la baadhi ya mashamba yaliyouzwa na diwani huyo na kwamba wakati wakiwa katika mashamba hayo, ndipo diwani na viongozi wenzake walionyesha mipaka ya maeneo hayo yakiwamo yaliyouzwa na diwani huyo huku akikiri kuuzwa kwa baadhi ya maeneo kwa wananchi wa Kata ya Ziba.

"Kwa kweli mimi nimeshangaa sana kwani nimeona hadi nyaraka za mauziano ambapo hadi picha ya diwani ipo kwenye karatasi hizo, hivyo basi TAKUKURU hawajamuonea wana haki ya kuwabeba," alisema.

Mwagara alisema baada ya kuona maeneo yaliyouzwa, maafisa hao waliondoka na viongozi hao kwenda Igunga kwa ajili ya mahojiano zaidi na hadi sasa wanashikiliwa kwenye kituo cha polisi Wilaya ya Igunga.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, Benjamin Sperto, alisema mashamba anayotuhumiwa kuuza diwani wa Kata ya Iborogero ni ya Wizara ya Mifugo ambayo yalitengwa na serikali kwa ajili ya kufanyia shughuli za wanyama kazi.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Igunga, Mafunda Ntemanya alikiri kukamatwa kwa diwani huyo na wamekuwa wakipokea malalamiko mengi toka kwa wananchi wa kata hiyo dhidi yake.

Alisema licha ya kumkanya mara kwa mara kutokujihusisha na tabia ya kuuza mashamba ya serikali pamoja na vitendo vya rushwa, lakini amekuwa mgumu kuelewa na tayari amemjulisha Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora kukamatwa kwa diwani huyo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tabora, Mussa Chaulo, alisema kwa sasa hawezi kuzungumzia suala hilo kwa kuwa wanaendelea na uchunguzi.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Costantino Mbogambi, alithibitisha kuwashikilia viongozi hao watano akiwamo Diwani wa Kata ya Iborogero na TAKUKURU waliwapeleka Kituo cha Polisi Igunga kwa ajili ya kuwahifadhi.

# Samia aridhia maji Ziwa Victoria kufikishwa Ushetu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameridhia ombi la kuanza utekelezaji wa kufikisha mradi wa maji ya Ziwa Victoria kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga hadi Halmashauri ya Ushetu ili wananchi wapate majisafi na salama.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso aliwaambia wananchi wa Kata ya Chona, muda mfupi kabla ya kuzindua mradi wa maji katika kijiji cha Busenda, uliotekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na chanzo chake ni kisima kirefu chenye urefu wa mita za ujazo 115 ambacho kina uwezo wa kutoa lita 5,800 kwa saa.

Alisema, amefanya mawasiliano na watendaji wa Wizara ya Maji na tenda ya utekelezaji wa mradi huo imeshatangazwa na itaendelea kutangazwa kwa muda wa siku 30 na mkandarasi atakayepatikana atakuja naye kumtambulisha kwa wananchi ili aanze kazi.

Aweso alisema, wakati serikali ikiendelea na mchakato wa kumpata mkandarasi atakayetekeleza mradi huo, kwa sasa wanatakiwa kuendelea kutumia maji katika mradi iliyotekelezwa na RUWASA ili kuepuka magonjwa ya mlipuko.

"Rais Samia Suluhu Hassan ujio huu hapa Ushetu anaufahamu na kaniagiza niwaambie kuwa ameridhia ombi la kuanza utekelezaji wa kufikisha maji ya Ziwa Victoria kutoka Manispaa ya Kahama hadi hapa Ushetu hivyo muda wowote kuanzia sasa mradi utatekelezwa kwa sababu tenda imeshatangazwa," alisema Aweso.

Aidha, mradi huo umefika maeneo mbali mbali ikiwamo Mkoa wa Tabora na mkoani Singida.

Alisema itakuwa ajabu maji hayo kushindwa kufika Halmashauri ya Ushetu na kuwataka kuwa wavumilivu wakati serikali ikitafuta mkandarasi wa kutekeleza na haitachukua muda mrefu kwasababu ni agizo la Rais.

Mbunge wa Jimbo la Ushetu Emmanuel Cherehani, alilazimika kupiga magoti na kumuomba Waziri Aweso aweze kufikisha kilio cha ukosefu wa maji ya uhakika Ushetu kwa Rais, lakini alipata majibu ya matumaini ya Rais Samia kuridhia utekelezaji wake.

Alisema, Mkoa wa Shinyanga una halmashauri sita, tano zina maji ya Ziwa Victoria isipokuwa Halmashauri ya Ushetu inayotumia maji ya visima, kati ya 20 ni kata 11 ambazo hazina huduma ya maji na wananchi wake wanatumia ya madimbwi hali inayoweza kusababisha kuwapo mlipuko wa magonjwa.

Mkazi wa kata ya Chona Sinfuroza Samweli alisema, awali walilazimika kutumia maji ya majaruba ya mpunga hasa kwa kipindi cha mvua ya masika kutokana na visima wavyochimba kukauka kipindi cha kiangazi.

Pia, wanafunzi hasa wa kike hukosa masomo kwasabau ya kuambatana na wazazi wao kutafuta majisafi na salama, na kuomba mchakato wa kumtafuta mkandarasi wa ujenzi wa mradi wa maji ya Victoria Kahama-Ushetu usichukue muda mrefu.

MAKALA MAALUM

## BAADA AGIZO LA RAIS KWA TRC

# Mkasa ‘treni ya Mwakyembe’ kuondoa abiria saa saba usiku



**Na Mwandishi Wetu**

MIEZI miwili tangu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila kuingilia kati kasoro kwenye ‘daladala’ za Shirika la Reli Tanzania (TRC), juzi usiku hali hiyo imejitokeza tena Stesheni ya Gerezani, abiria kutelekezwa hadi saa 6.50 usiku bila ufafanuzi.

Watarajiwa hao wa safari iliyopaswa kuondoka saa 4.30 kwenda Pugu, waliamua kuvamia ofisi za stesheni wakidai wamechoshwa, huku anayedaiwa msimamizi wa stesheni Gerezani akatoweka, akimtwisha jukumu ofisa wa polisi kutoa majibu na kuwatuliza.

Ni tukio linaloshabihiana na la Novemba 9 mwaka jana, treni ilipopata mkasa kuelemewa abiria, wapo waliodandia kwenye kichwa. Nipashe iliporipoti, Mkuu wa Mkoa Chalamila, akaingia kati akiwa na safu ya menejimenti ya TRC, akihitimisha kwa maagizo makubwa ya maboresho.

Chalamila aliyeweka wazi kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyeliona hilo, siku iliyofuata asubuhi akasafiri na menejiment ya TRC hadi Pugu na kurejea Grezani, alikokusanya malalamiko, kilichotokea juzi usiku kikiwa kimojawapo alichotolea maagizo ya maboresho.

Mkasa wa juzi usiku ulianza kwa abiria waliotarajiwa kuondoka saa 4.30 usiku, walisubiri treni tarajiwa Pugu huku wakitaarifiwa kwenye kipaza sauti ‘treni kutoka Pugu inakuja sasa hivi mtaondoka mara moja.’ Hata hivyo, ilifika mahali hapo saa 5.20 usiku.

Abiria walipoingia kwenye mabehewa, treni ikaendelea kubaki stesheni, baadhi wakaamua kuondoka kutafuta usafiri mbadala.

Vilevile, Nipashe ikashuhudia stesheni Gerezani abiria wa treni inayokwenda Moshi waliodai kuwapo tangu asubuhi, wakiwapo hadi muda huo usiku.

Kukiwapo vuguvugu abiria wa daladala kukasirika, kipaza sauti kikaendelea kutangaza ‘abiria endeleeni kuwa wavumilivu tutaondoka’. Ilipotimu saa 6:00 usiku, wengi wakihoji kitendawili cha kukwama kuondoka, baadhi wakavamia ofisi kutafuta majibu, wengine wakihitaji kurejeshewa nauli zao.

Hata hivyo, hapakuwapo ufafanuzi, kila mtendaji akikwepa kutoa majibu ya moja kwa moja. Pia, muda mfupi kabla ya ofisi kuvamiwa, anayedaiwa msimamizi wa stesheni alipotakiwa kutoa ufafanuzi, akawajibu ‘mimi sijachukua fedha zenu’ na akatoweka, hakuonekana tena.

Awali msuguano ukipamba, treni inayokwenda Moshi nayo ilikuwa haijulikani muda wake kuondoka. Abiria wakiwa nje ghafla saa 5: 30 usiku wakatangaziwa wajiandae kuondoka na baada ya dakika 20 safari ikaanza, kukiwapo dai lisilo la wazi’ ilikuwa imewazibia abiria wa Pugu.’

Sintofahamu ya abiria wa Pugu ikiwa imepamba moto, ofisa polisi mwenye cheo cha mrakibu msaidizi (ASP), aliamua kubeba dhamana kuwajibu wateja, pia kuwatuliza katika ufafanuzi ambao, hata hivyo haukuwaridhisha.

Baadaye Nipashe ikabaini hata askari huyo ASP alilazimika kujitolea kushughulikia mkasa wa treni ya Pugu, akiachwa na treni aliyotarajia kusafiri nayo kikazi kwenda Moshi kutokana na hali iliyotawala.

Shinikizo la abiria lilipozidi, safari ya treni ya kwenda Pugu ikaanza saa 6:50 usiku. Nipashe ikiendelea kufuatilia safari hiyo, treni iligeuza Pugu kurejea Gerezani saa 8:00 usiku, muda usio na abiria kwa matarajio ingefika Gerezani saa 8:40 usiku.

### WATUMISHI

Sintofahamu haikushia kwa abiria pekee, hata watumishi wa treni ndani na nje ya ofisi za TRC Gerezani, wakawa wanang’aka kunyoosheana vidole, ‘wanajitakia hawa’, tuliwaambia....’

Katika kinachonekana kususa, watumishi kama vile wakata tiketi ‘TT’ na Inspekta kwenye mabehewa safari ya Pugu hawakuwapo, abiria walibaki wenyewe, kinyume cha kanuni za TRC na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), dai lao kuu likitajwa wamechoka.

Vilevile, Nipashe ikashuhudia ndani ya usafiri huo maarufu ‘Treni ya Mwakyembe’ kutokana na kuchelewa usiku, hapakuwapo abiria wanaopanda katika vituo vya njiani kama vile: Ilala Bungoni, Buguruni, Vingunguti, Majani ya Chai/Kipawa, Uwanja wa Ndege, Majumba Sita, Mombasa na Gongo la Mboto.

Kasoro zilionekana mapema, hata katika ratiba tangu asubuhi treni hiyo inayotoka Pugu saa 2:20 asubuhi, ikiwa ni safari ya pili, juzi ilifanya hivyo wastani wa saa 3:25 ndipo ikaanza safari asubuhi Pugu.

Vilevile, usiku treni hiyo iliyochelewa kufika Gerezani saa 5:20 ikitoka Pugu inazua maswali, kwa kuwa awali ilifika stesheni huko saa 2:15 kutoka Pugu. Ni muda inayopaswa kuondoka kwenda Pugu.

Kurejea kwake ilichelewa kupindukia, kulinganisha na ratiba yake, bila taarifa, getini wakiendelea kukata tiketi. Saa 4:30 usiku kwa ratiba ni muda wa kuondoka kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa kwa umma na Mkuu wa Mkoa Chalamila, safari ya mwisho kwenda Pugu ni saa 5:30, ikianza safari kurejea kulala Gerezeni, kabla ya kuanza siku inayofuata saa 10: 50 alfajiri.

Nipashe ikashuhudia mkasa unaonyooshewa kidole cha kukosekana umakini, pale mabehewa machahe ya usafiri ya kwenda Ubungo yakipangwa, katika hali inayotarajiwa kutokuwa makini ikaleta shida.

Mtendaji huyo akifyatua kifaa cha kubadili reli mahali pake, inadaiwa hakufanya kwa umakini hata kusababisha behewa mojawapo kusogea vibaya, ikazama kwenye mchanga na hadi juzi usiku, treni hiyo ilikuwa imekwama.

### JICHO LA CHALAMILA

Katika ukaguzi wake Novemba 9, 2023, Mkuu wa Mkoa Chalamila alifuatana na Katibu Tawala Rehema Madenge na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo.

Vilevile, alifuatana na menejimenti ya TRC ikaongozwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Amina Lumuli, Mkurugenzi wa Uendeshaji, Focus Makoye, Kamanda wa Polisi Reli, Sebastian Mbuta, pia uongozi wa Wakala wa Barabara (TANROADS) na LATRA.

Makosa yaliyojiri, kati ya zaidi ya 10, baadhi ya hayo ni: treni kutozingatia ratiba; kutotolewa risiti, pia abiria kutorejeshewa fedha penye mkasa kama wa juzi; hakuna sehemu za kujisitiri na mvua /vyoo, pia nidhamu mbaya na uonevu wa polisi, mabehewa machache ya wanafunzi, na safari kuwa chache, hasa siku ya Jumamosi.



## RIVACU yamwangukia Samia kuhusu shamba la Dareda

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

HOFU ya kutwaliwa na serikali eneo la ardhi yenye ukubwa wa hekari 2,020 za shamba la Dareda lililoko wilaya ya Babati mkoani Manyara, linaipasua kichwa Bodi Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Manyara (RIVACU).

Hivyo wamemuomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuingilia kati mpango huo ili kuwasaidia wanaushirika wasinyang'anywe ardhi hiyo.

Jana, Mwenyekiti wa Bodi ya RIVACU, Yuda Sulley, alisema wanaamini serikali ipo kwa ajili ya kulinda na kutetea ushirika, hivyo wana kila sababu ya kumwomba Rais Samia awasaidie shamba hilo lisimegwe na kugawanywa kwa wananchi.

Aidha alisema kuwa shamba hilo lina ukubwa wa ekari 4,961 na lina aina tatu za umiliki.

"Timu ya mawaziri wanane ilipokuja ilitoa mapendekezo ya kumegwa shamba hilo hekari 2,941 ili zigawiwe kwa wananchi wa vijiji vya Dohomu, Endasago na baadhi wa Kijiji cha Dudiye,"alifafanua zaidi.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo eneo hilo waliloridhia litwaliwe ni karibu asilimia 60 ya eneo lote, hivyo wao watapaswa kubaki na ekari 2,020 sawa na asilimia 40 ya shamba lote.

Sulley alisema kuwa licha ya kubaki na eneo dogo wanashangaa eneo la Endomundo, kupendekezwa hekari 110 kubadilishwa matumizi baada ya hati yake kufutwa.

Alisema iwapo hati yake ya umiliki itafutwa na kubadilishwa matumizi, uchumi wao utayumba kwa kuwa eneo hilo ndilo linalotumika kustawisha zao la kahawa kwa wingi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko (Giba-AMCOS), Michael Tsaxara, alisema shamba hilo halina mgogoro wowote, badala yake watu wanataka kuleta taharuki.

Alipoulizwa kuhusu madai hayo, Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema hakuna mtu aliyekwenda kugawa shamba hilo, badala yake wananchi waliitwa kwenda kuonyeshwa mipaka, ili wajue eneo lililofutwa na serikali.

# Ukichanganya viuatilifu na bidhaa zingine faini mil.500/-

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MAMLAKA ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA) imewaonya wafanyabiashara wa viuatilifu wanaochanganya na bidhaa zingine pamoja na kufungua maduka yao katika makazi ya watu na masoko.

Imesema yoyote atakayebainika anafanya hayo atakumbana na adhabu kali ikiwemo kutozwa faini ya Sh. 50,000 hadi Sh. milioni moja kwa mtu na Sh. milioni 10 hadi Sh. milioni 500 kwa kampuni au kwenda jela miaka mitatu.

Ofisa Sheria Mwandamizi wa TPHPA, Elizabeth Swai, aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika mafunzo ya wakaguzi wa viuatilifu kutoka katika mipaka yote nchini, ambayo yanaendelea katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Alisema wakaguzi hao wanapaswa kushughulikia tatizo hilo kwa kuwa wana meno ya kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria.

Mafunzo hayo yanatokana na utekelezaji wa mradi wa kujenga uwezo unaohusiana na mikataba ya kimataifa ya mazingira (ACP MEAs III), unaoratibiwa na TPHPA na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), kwa ufadhili wa Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU).

"Kwa mtu atakayekutwa amevunja Sheria ya Afya ya Mimea na Viuatilifu, sheria zetu zimegawanyika mara mbili. Kuna adhabu kwa mtu binafsi, na adhabu kwa kampuni.

"Adhabu hizo ziko zimetajwa katika Kifungu cha 59 cha Sheria ya Afya ya Mimea, Namba 4 ya Mwaka 2020. Adhabu kwa mtu binafsi faini ya kuanzia Sh. 50,000 mpaka Sh.milioni 10, au kifungo cha miaka isiyozidi mitatu jela.

Na kwa kampuni, adhabu yake ni kuanzia Sh. milioni 10 mpaka Sh. milioni 500 au miaka mitatu jela, endapo atashindwa kulipa hiyo faini. Licha ya adhabu hizo, TPHPA inaweza ikamfungia kabisa mfanyabiashara aliyekutwa na kosa hilo na endapo atakutwa na viuatilifu ambavyo havikidhi matakwa, TPHPA inaweza ikatoa notisi kwamba anapaswa ateketeze kwa gharama zake mwenyewe, baada ya kupata maelekezo kutoka NEMC."

Kwa mujibu wa Swai, Kifungu cha 50 cha Sheria ya Afya ya Mimea, namba 4 ya mwaka 2020, ambacho kinazungumzia masuala ya usafirishaji, kimeelekeza kuwa mtu yeyote anayesafirisha viuatilifu, hapaswi kuvichanganya na vitu vingine, aidha iwe vyakula, nguo na vitu vingine vinavyoendana na hivyo.

Vilevile, amefafanua kuwa Kifungu cha 51 cha sheria hiyo, kinaelekeza kwamba maduka ya viuatilifu au sehemu yeyote ya kuhifadhia viuatilifu, hayapaswi kuwa karibu na shule, hospitali, vyanzo vya maji au maeneo ya kuuza vyakula na sokoni.

Mkurugenzi Mkuu wa TPHPA, Prof. Joseph Ndunguru, akizungumza na wakaguzi 32 wa viuatilifu nchini alisema: "Mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo wataalam ili waweze kufanya kazi za ukaguzi wa viuatilifu. Lengo kuu ni kwamba unapokuwa na ukaguzi wa viuatilifu, maana yake unachangia ule mkakati wetu wa kuwa na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu, ili kulinda afya ya binadamu lakini pamoja na mazingira.

"Tunaendesha haya mafunzo TPHPA, kwa kushirikiana na wabia wa maendeleo ambao ni FAO na EU (Umoja wa Ulaya), ambao wamechangia katika kutoa fedha za kuendshea mafunzo haya."

Prof. Ndunguru ameeleza kuwa faida kubwa ambayo itatokana na mafunzo hayo ni kuongezeka kwa tija katika mazao na kuboresha masoko ya mazao kwa maana ya kuwa na mazao yenye kiwango kikubwa cha ubora, ambacho kitauzwa nje na kuliingizia taifa pato la fedha za kigeni.

Kwa Tanzania mradi huo unatekelezwa katika mikoa sita ambayo ni Dar es Salaam (Kigamboni), Morogoro (Kilosa), Iringa (Kilolo), Mbeya (Mbarali), Arusha (Karatu) na Kilimanjaro (Same).



Mkuu wa Polisi Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Hadija Sokolo (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa wilaya hiyo, Leonard Bandola (kulia), baada ya kufanya majaribio ya kifaa kipya cha kutambua madeni ya makosa ya usalama barabarani juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# EACOP yawakumbuka waathirika maporomoko Hanang'

**Na Mwandishi Wetu,** HANANG'

MENEJIMENTI ya Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), imewakumbuka waathirika wa maporomoko ya tope wilayani Hanang' mkoani Manyara, baada ya kutoa msaada wa mifuko 1,000 ya saruji, kwa ajili ya ujenzi wa makazi mapya.

Maafa hayo yaliyotokea Desemba 3, mwaka 2023, yalisababisha vifo vya watu 89 na kujeruhi wengine 139 katika Mji wa Katesh, vijiji vya Jorodom, Ganana, Katesh, Dumbeta, Gendabi, Sarijandu, Arukushay na Sebasi.

Katika maporomoko hayo kaya 207 zilizokuwa na wakazi 322, zimepoteza makazi katika maeneo hayo.


Kabla ya kukabidhi saruji hiyo kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa EACOP (Tanzania), Catherine Mbatia, alisema mchango huo walioutoa, ni ushuhuda wa dhamira yao katika kusaidia wenye uhitaji.

"Sisi ECOAP tunaamini katika dhamira ya uwajibikaji kwa jamii. Kwa sababu tunatambua maafa hayo yamegharimu maisha ya watu na kusababisha uharibifu mkubwa katika mashamba na mamia ya watu wamepoteza na kuhama makazi yao. "Katika kukabiliana na maafa haya, EACOP imechangia mifuko 1,000 ya saruji ili kutoa msaada muhimu kwa waathirika wa mafuriko katika Wilaya ya Hanang'. Saruji hii itatumika kusaidia ujenzi wa nyumba zaidi ya 101 ambazo serikali imepanga kuwajengea waathirika."

Mbatia alisema EACOP inaamini katika nguvu na kuchukua hatua kwa pamoja, hivyo imedhamiria kutumia rasilimali zake, kuchangia ipasavyo katika kurejesha maisha ya kawaida na kujenga upya jitihada za wilaya hiyo.

Baada ya kupokea saruji hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alisema maafa hayo yameiacha jamii ya watu wa Hanang' katika uhitaji mkubwa, kwamba msaada huo umekuja kama mwanga wa matumaini katika nyakati hizi za uhitaji.

...Tunashukuru kwa mwitikio wao wa kusaidia mpango wa serikali wa kujenga upya na kurejesha maisha ya kawaida ya jamii kutokana na janga hili."



HABARI KANDA YA ZIWA

# Aweso awajia juu MWAUWASA danadana kuunganisha maji

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kuacha visingizio katika suala la kuwaunganishia maji wananchi, baada ya mradi wa maji Butimba kukamilika.

Alitoa agizo hilo juzi alipoambatana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti wakati wa ukaguzi wa mradi huo ambao unatajwa kufikia asilimia 100 ya utekelezaji wake.

Waziri Aweso alisema kama wizara hawatokuwa tayari kupokea sababu zozote juu ya kuchelewa kuwaunganishia watu maji wanaotakiwa kwa muda mfupi, lengo likiwa ni kuwawezesha kunufaika na huduma hiyo kwa utoshelevu.

Alisema kukamilika kwa mradi huo ni tija kwa wananchi ambao walikuwa wanakabiliwa na uhaba wa maji, kwani uhitaji wao ulikuwa lita milioni 172.

Aweso alidokeza lengo la Wizara ya Maji ni kuendelea kujenga miradi ya kimkakati na kutatua matatizo ya maji katika maeneo ya mijini na vijijini na hivi sasa wanamiradi katika miji 28 katika maeneo yaliyokuwa na tatizo la maji na kwamba wanatumia chanzo toshelevu ili kuhakikisha wanatatua matatizo hayo ipasavyo. Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Daniel Sillo, alisema kamati inapitisha bajeti ya Wizara ya Maji zinazotumika katika ujenzi wa miradi mbalimbali ya serikali katika sekta zote.

Alisema hawatakuwa kikwazo bali watahakikisha wanasimamia miradi ya maji iliyopo na inayoanzishwa katika maeneo mbalimbali nchini, huku dhamira yao ni wananchi kupata majisafi na salama."Kazi nzuri imefanyika, tumeridhika na kinachoendelea hapa. Kwenye mradi wa Butimba utakidhi mahitaji ya wananchi wa Mwanza nampongeza Rais kwa dhamira yake ya dhati ya kumtua mama ndoo kichwani," alisema Sillo. Awali akitoa taarifa ya mradi huo, Mhandisi Selestine Mahubi alisema utekelezaji wake umebakiza hatua kama nne kwa ajili ya kuchukua maji ziwani na baada ya kuyachukua yatapelekwa kwenye mtambo kisha kwenye matangi na baada ya hapo yanaenda kwa wananchi.

## Kitete yaweka mikakati kudhibiti vifo mama, mtoto

**Na Halima Ikunji,** TABORA

HOSPITALI ya Rufani Mkoa wa Tabora Kitete imeweka mikakati ya kuendelea kutoa huduma muhimu zikiwamo za afya ya uzazi kwa mama na mtoto, ili kudhibiti vifo vitokanavyo na uzazi.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Nassoro Kaponta kwenye hafla ya kukabidhi gari mbili ikiwamo gari ya wagonjwa katika hospitali hiyo.

Gari hizo zilizokabidhiwa na Mbunge wa Tabora Mjini, Emmanuel Mwakasaka.

Dk. Kaponta alisema jitihada na juhudi zimeendelea kufanyika kwa weledi mkubwa, lengo kuu likiwa kudhibiti na kupunguza vifo vya watoto wachanga.

Alisema Mkoa wa Tabora una jumla ya vituo vya kutolea huduma 406 ikiwa ni pamoja na hospitali 15, vituo vya afya 43, zahanati 341.

Dk.Kaponta alisema kuwa vituo 328 sawa na asilimia 80 inajumuisha hospitali nane, vituo vya afya 34 na zahanati 286 ambavyo ni vya serikali.

Alisema vituo 343 sawa na asilimia 84 kati ya vituo 406 vinatoa huduma za kliniki ya wajawazito na watoto.

Dk.Kaponta alitaja Mkoa wa Tabora kuwa una wakazi zaidi ya milioni 3.39 huku kati yao kinamama wenye umri wa kujifungua kuanzia miaka 15 hadi 49 ni 791,379.

Alisema katika kipindi cha Januari hadi Oktoba 2023 kinamama 104,309 walijifungua, kwamba kati yao 101,856 walijifungulia vituo vya kutolea huduma za afya.

Aidha alisema kinamama 2,453 sawa na asilimia tatu walijifungulia njiani kabla ya kufika vituoni na 845 walijifungulia nyumbani na 101 walijifungulia kwa wakunga wa jadi.

Dk. Kaponta alisema pamoja na kuwapo sababu mbalimbali ya baadhi ya kinamama wajawazito kutojifungulia vituoni imebainika kuwa asilimia tatu wanashindwa kuwahi kupata au ukosefu wa usafiri wa uhakika.

Vilevile alitaja ukosefu wa magari ya kubeba wagonjwa hali inayochelewesha baadhi yao kukosa huduma za haraka, huku akitaja mkoa huo kuwa una gari 32 kati ya 60 yanayohitajika sawa na asilimia 53.3.




Waziri wa Maji, Juma Aweso (kulia) na Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, wakifungua bomba kuzindua mradi wa maji wa Kijiji cha Busenda, Kata ya Chona, Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga jana, uliotekelezwa na RUWASA kwa Sh. milioni 344.4. Wengine ni wakazi wa kijiji hicho. **PICHA: SHABAN NJIA**

# RUWASA watekeleza miradi kwa mil.344/-

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MRADI wa maji uliotakiwa kutekelezwa kwa Sh. milioni 456.321 umetekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa gharama ya Sh. milioni 344.480, huku Sh.milioni 111.841 zikiwa zimeokolewa.

Hatua hiyo imemfurahisha Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na kuupongeza uongozi wa RUWASA Mkoa wa Mwanza kwa utekelezaji wa mradi huo uliopo katika Kijiji cha Busenda Kata ya Chona Halmashauri ya Ushetu.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa mradi huo, Meneja wa RUWASA Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Julieth Payovela alisema utekelezaji ulianza Machi 10, 2023 na utakamilika Septemba 5, mwaka huu.

Alisema, mradi ulitakiwa kutekelezwa kwa Sh. milioni 456.3 lakini wao waliutekeleza kwa Sh.milioni 344.4 na kubakiza zaidi ya Sh.milioni 100 fedha zilizotokana na mpango wa malipo kwa matokeo.

Payovela alisema kukamilika kwa miundombinu ya maji katika Kijiji cha Busenda wakazi 3,551 watanufaika na huduma ya majisafi na salama.

Alisema mpaka sasa wateja 26 wameshaunganishiwa huduma ya maji nyumbani na kazi ya kuunganisha maji linaendelea na hakuna malalamiko yoyote yanayoripotiwa.

Diwani wa Kata Chona, Mabala Mlolwa alisema awali wajawazito waliokuwa wanakwenda katika Zahanati ya Chona kupata huduma ya kujifungua walilazimika kwenda na ndoo ya maji.

Alisema lakini kwa sasa adha hiyo haipo tena na ni baada ya mradi huo kufika zahanati na maji yanatoka.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani alisema mradi umekamilika lakini haujafika katika vitongoji viwili vya Imambo "A" na "B" na kuomba kiasi kilichobaki wakati wa utekelezaji wa mradi kitumike kufikisha maji kwenye vitongoji, hivyo ili kuwanusuru wananchi kuendelea kutumia maji yasiyo safi na salama.

Waziri Aweso alisema, Wizara ya Maji inahitaji viongozi wa namna hiyo wanaotekeleza miradi kwa weledi mkubwa bila uingiza tamaa ya kujipatia fedha, kwani wangekuwa wengine wangeweza kugawana chenji zilizobaki lakini wao wameweka matumizi wazi, kuwataka wengine kuiga mfano huo.

ama
ALHAMISI JANUARI 11, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

## Kinababa wanavyotapeliwa biashara ya kuwapa ujauzito wahitaji India



## Mbadala wa elimu ulivyorahisisha vita vya bangi kwa vijana Arumeru

Ukurasa 12

# Staili ya Rais kuwekeza PPP ndani safari inayoipaisha Sekta ya Afya

•Darasa kutoka NHIF, hospitali kukaa meza moja

**Na Mwandishi Wetu**

JUZI akiwa kisiwani Pemba, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akataja jambo la kipaumbele chake kiutawala kinajumuisha huduma za ustawi, ikiwamo tiba.

Hapo akasisitiza afya iwe kipaumbele zaidi ya hatua kubwa ya sasa kueneza juhudi zinazofanywa katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

Ndani ya eneo hilo, serikali ya Muungano chini ya Rais Dk. Samia imekuwa ikitenda kwa kushirikisha sekta binafsi kupitia sera na sheria inayohuisha sekta binafsi, Mpango wa Ubia wa Sekta Rasmi na Umma (PPP), ambao ulianza kutumika katika zama serikali ya awamu ya tano.

Uhusiano huo katika sekta ya afya nchini ulishuhudiwa hivi karibuni, Mfuko Bima ya Afya na hospitali binafsi zilipokaa meza moja kuhusu maudhui mapya ya binama ya afya, hata utekelezaji wake ukasitishwa kwa muda.

Hayo kwa kina, yameshuhudiwa kwenye huduma zote za kiafya kinazihitaji mwongozo wa kisera kutoka afya, sekta binafsi hushirikishwa kikamilifu.

Mfano sahihi hai katika hizo, hakuna mipaka katika matumizi ya huduma za afya za NHIF, baina ya hospitali binafsi na umma, hali kadhalika kwenye huduma za chanjo za lazima na dharura.

Mnamo wiki mbili na nusu zilizopita, mwishoni mwa mwaka jana, taasisi ya Doris Mollel Foundation, kwa kushirikiana na msanii Barnabas, wakatoa vifaa tiba kwa ajili ya kuanzisha wodi ya watoto wachanga mahututi na njiti, katika Hospitali ya Masiwani, jijini Tanga.



Hafla inayohusu taasisi binafsi kutoa vifaa tiba hospitalini. **PICHA: MTANDAO.**

Vifaa hivyo vyenye thamani milioni 35, vinatajwa kujumuisha vitanda viwili vya hospitali; mashine ya mwanga kumtibu mtoto na maradhi manjano, nyingine inamsaidia kupumua; na puto la kumsaidia kupumua.

Mengine ni mashine ya joto, magodoro 10 ya kuongeza joto la motto, mashine inayotoa dawa kusaidia kupumua, na mashine inayopima kiwango cha oksijeni kwa mtoto.

Aidha kunatajwa vifaa pampu tano za miguu, pampu tatu za umeme, mashine mbili za kutengeneza hewa oksijeni, na idadi kama hizo vifaa vya kupima uzito wa watoto.

Mbunge wa Tanga Mjini na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anataja mwelekeo wa serikali uliopo kwa afya ya uzazi mama na mtoto ni kujikita kuhudumia bora watoto wachanga, hasa wanaozaliwa kabla ya wakati, kupunguza vifo vyao.

Hapo anaitaja Serikali ya Awamu ya Sita inajikita kitakwimu vifo hivyo kupunguza kufikia vifo 12 vya watoto wachanga kwa kila vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2030, kutoka vifo 24 vya sasa.

Inatajwa kuna tafiti zinaonyesha nusu ya watoto wachanga asilimia 50 wanaopoteza maisha, wanaposafirishwa umbali mrefu, kwa sababu ya kupoteza joto la mwilini.

**AWAMU VI INAVYOWAFIKIA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya, imetamka itajenga kituo kipya cha afya katika Kijiji cha Gendabi wilayani Hanang, Manyara kusaidia upatikanaji wa huduma za afya karibu na wananchi.

Ni kauli ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Manyara, kukagua upatikanaji dawa na kutoa pole kwa wananchi wa eneo lililoathirika na maporomoko ya matope.

"Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais Tamisemi, tutajenga kituo kipya cha Afya katika makazi mapya yaliyotengwa na mkoa, kwa ajili ya wananchi walioathirika na maporomoko hayo..." anatamka Waziri Ummy

Anasema fedha hizo zimetolewa na Rais Dk. Samia, wapelekewe wananchi katika eneo hilo jipya la Wareti, kutakapojengwa kituo kipya cha afya, kununuliwa vifaa tiba vya kutosha na watumishi.

Waziri Ummy akaahidi kupelekwa magari matatu ya kubeba wagonjwa, ikiwa ni tofauti na zaidi ya magari 900 ya mgao yaliyotawanywa nchini na TAMISEMI.

Vilevile, Waziri Ummy akasema, majeruhi watano wa mmomonyoko wa udongo waliosalia kati ya 139 waliyofikishwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, wataendelea kuhudumiwa kwa gharama za Serikali.

"Rais Samia amekatisha ziara yake nchi za nje amekuja kwenu ili kuwa pamoja nanyi na sisi kama Wizara ya Afya tupo tayari kutimiza mahitaji mengine yote yatakayohitaji," akatamka Waziri Ummy.

MAZINGIRA

# Mbadala wa elimu ulivyorahisisha vita vya bangi kwa vijana Arumeru



Moja ya shamba la mkazi wa Kijiji cha Kisimiri, Kata ya Uwilu, likiwa limelimwa maharage, ambalo zamani lililimwa bangi. **PICHA ZOTE: ZANULA MOLLEL**

Gunia za bangi na mbegu zake kilo 310, zilizokamatwa huko Arumeru, tayari kwa ajili ya kuchomwa moto.

**Na Zanura Mollel**

ELIMU ni mchakato wa kupata maarifa, stadi, maadili na ufahamu. Inaweza kugawanywa katika makundi kadhaa kulingana na viwango vyake na malengo yake.

Makundi hayo ni pamoja na elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, ya juu, na ya mafunzo ya ufundi.

Vilevile katika makundi yake makuu, kuna elimu rasmi na isiyo rasmi. Inapokuwa rasmi, huwa na mwongozo au mtaala unaotoa mwelekeo wa kufuata na unatambuika rasmi, ndilo kuna simulizi zaidi za kuhitimu na kupata vyeti.

Hapo usomaji wake una makundi na wanaopata vyeti, vilevile maandalizi kwa ajili ya majukumu mbalimbali katika jamii.

**DAWA ZA KULEVYA**

Kuhusu athari za dawa za kulevya, elimu yake inalenga kutoa maarifa kuhusu madhara yanayoweza kutokea kutokana na utumiaji wake. Hiyo inajumuisha athari za kiakili, pia afya ya mwili.

Ni eneo linalosisitiza kutumia dawa za kulevya na uharibifu wa mfumo wa neva mwilini na akili, kuathirika uhusiano na jamii na kudhuru maisha ya mtu.

Kupitia elimu, jamii inalengwa kuelewa madhara ya dawa za kulevya, ikihamasishwa hatua za kuzuia na kutibu mabaya yake.

Ni elimu inayotolewa shuleni, kazini au kupitia kampeni za umma kujenga uelewa na kuchangia juhudi kupunguza matumizi na athari zinazosababishwa na dawa hizo.

"Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini(DCEA), imejikita zaidi katika kutoa elimu kwa wananchi badala ya kutumia nguvu, ikiwa kuwaelimisha athari zake, lakini kuwakumbusha sheria za nchi zinasemaje," anatamka Kamishna Jenerali Arates Lyimo.

"Jitihada za serikali ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuepuka matumizi ya dawa ya kulevya ikiwamo bangi na mirungi, ambazo athari zake ni kubwa kama kupunguza nguvu za kiume, kukosa usingizi na kuharibu mfumo wa fahamu. Hata hivyo, nchi nyingi zenye usambazaji na utumiaji mkubwa wa dawa hizo, hakuna amani," anatamka Dk. Peter Mfisi, Kamishna wa Kinga na Tiba kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania.

**MKOA WA ARUSHA**

Arusha ni mkoa wenye wakazi 2,356,255, waliogawanyika; wanaume 1,125,616 na wanawake 1,230,639, wanaoishi katika wilaya sita ikiwamo Arumeru. Vilevile kuna halmashauri saba.

Kamishna Dk. Peter Mfisi anaitaja Arusha, ni miongoni mwa mikoa nchini kunakolimwa zao la bangi kwa misingi ya biashara.

Anasema hadi sasa, kuna utafiti na mradi wa serikali kusaka mazao katika maeneo yaliyoathiriwa na kilimo hicho, huku Dk. Mfisi akifafanua 'mikoa inayostawisha bangi kama zao la biashara ni Arusha, Morogoro, Mara, Iringa na Njombe."

> "Maji wanatumia kutoka vyanzo vya Hifadhi ya Arusha, ni 'machache sana' hayakidhi mahitaji ya wananchi, wakati mwingine wanyamapori uharibu miundombinu iliyopo na 'kupelekea' kukosekana maji katika jamii. Hakuna bajeti yoyote tuliyotengewa hadi sasa ya huduma za maji," anasema Urio.

**ZAO LA ELIMU**

Diwani wa Kata ya Uwilu, Dawson Urio, anaiambia Nipashe kwa njia ya simu, akieleza wakazi wa Kisimiri Juu wamepunguza kwa kiasi kikubwa kilimo cha bangi kutokana na elimu waliyopatiwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kuzuia Dawa za Kulevya, pia mikakati waliojiwekea kama kijiji.

"Kijiji tulikubaliana atakayebainika anayelima bangi, atatozwa faini shilingi laki tano, lakini tuliteua wajumbe kila kijiji watu 20 wakufanya doria katika mashamba.

"Kisimiri Juu tulishawakamata waliokiuka makubaliano wakatozwa faini na mashamba yao yalifyekwa," anasema Diwani Urio.

Anataja changamoto inayowakabili, ni ukosefu wa majisafi na salama, pia miundombinu ya barabara, ikiwakwamisha shughuli zao za maendeleo katika kata hiyo na maeneo mengine yanayounganishwa na kijiji hicho.

Hata hivyo, anasemja serikali kupitia Mfuko wa Barabara (TARURA) imewaswesha shilingi million 48.5 za kutengeneza kilomita nne za barabara inayoanzia Oldonyosambu hadi Kisimiri Juu, hata hivyo mkandarasi hadi hajaanza utekelezaji uliotakiwa kuanza Novemba, 2023.

"Maji wanatumia kutoka vyanzo vya Hifadhi ya Arusha, ni 'machache sana' hayakidhi mahitaji ya wananchi, wakati mwingine wanyamapori uharibu miundombinu iliyopo na 'kupelekea' kukosekana maji katika jamii. Hakuna bajeti yoyote tuliyotengewa hadi sasa ya huduma za maji," anasema Urio.

**DCEA KANDA KASKAZINI**

Ofisa Elimu Jamii Kanda ya Kaskazini wa DCEA, Shabani Miraji, anasema kuanzishwa kwa ofisi ya kanda mnamo Septemba mwaka jana, kumesaidia kurahisisha shughuli za mamlaka katika utoaji elimu na kudhibiti dawa za kulevya.

Anafafanua kuwa operesheni hizo zilianza kikanda na mwezi uliofuata Oktoba kufanikiwa kudhibiti magunia 237 ya bangi kavu, zilizoandaliwa kusafirishwa, pamoja na kilo310 za mbegu za bangi katika vijiji hivyo.

Miraji anasema, pia wakatoa elimu ya madhara ya kuyatumia na biashara ya dawa za kulevya katika Shule ya Sekondari Kisimiri na Shule ya Sekondari Lesinoni, akinena: "Jumla ya wanafunzi 1442, walimu 59 na viongozi 25 wa vijiji hivyo walinufaika".

Anasema Desemba 20, mwaka jana ofisi hiyo kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama wilayani Arumeru, walifanya ziara ya kushitukiza katika vijiji hivyo, lengo ni kufanya tathmini ya kilimo cha bangi na elimu iliyotelewa kwa umma.

Hapo ikabainika mashamba yaliyokuwa yakijishughulisha na kilimo haramu cha bangi, wamiliki wamebadili mtazamo na kuanza kujikita katika kilimo cha zao la mahindi na maharagwe.

**RIPOTI YA UNODIC 2022**

Ripoti ya kimataifa ya mwaka 2022, iliyotolewa kuhusu dawa za kulevya ya Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Dawa na Uhalifu(UNODIC), inaeeleza kuwa uhalalishaji wa bangi katika sehemu kadha za dunia, unaonekana kuongeza kasi ya matumizi yake kila siku na athari zinazohusiana na afya.

"Amerika Kaskazini inaonekana kumeongeza matumizi ya kila siku ya bangi, hasa bidhaa zenye nguvu za bangi na hasa miongoni mwa vijana," inatamka ripoti, ikitajwa ongezeko la watu walio na shida ya akili, kujiua na kulazwa hospitalini.

Masoko haramu ya dawa za kulevya yatajwa kuwa na athari za kimaeneo, kijamii au kiwango cha mtu binafsi kwa mazingira.

Athari za kimazingira ni pamoja na ukataji mkubwa wa miti unaohusishwa na kilimo haramu, taka zinazozalishwa wakati wa utengenezaji dawa haramu za kemikali.

Pia zinapokuwa nyingi na utupaji taka unayoathiri udongo, maji na hewa moja kwa moja, vilevile huangukia viumbe, wanyama na kugusa mnyororo wa chakula kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

**AGIZO LA RAIS**

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ametaka kufanyike operesheni nchi nzima, lengo la kuhakikisha dawa za kulevya zinatokomezwa.

Kamishna Mkuu wa DCEA, Lyimo alifanya operesheni inayoitwa 'Tokomeza Bangi' kwa siku mbili wilayani Arumeru mkoani Arusha katika kijiji cha Kisimiri na Lesinoni na kufanikiwa kunasa gunia 731 za bangi kavu, pia kukateketezwa ekari 308 za mashamba yaliyokuwa yamelima zao hilo.

"Kijiji cha Kisimiri gunia 482 za bangi kavu zilikamatwa hekari 101 za mashamba zilifyekwa, Lesinoni gunia 249 za bangi kavu na kufyeka hekari 207," anatamka Kamishna Lyimo.

AFYA

# Kituo cha afya kipya chawapa unafuu kinamama safari km. 30

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

SERA ya Afya ya kila kijiji kuwa na zahanati, kata kuwa na kituo cha Afya, wilaya kuwa na hospitali na mkoa kuwa na hospitali ya rufani, inaonekana kuleta nafuu kwa wajawazito ikiondolea adha kutembea umbali mrefu kutafuta huduma sahihi za uzazi.

Katika kata ya Kinaga, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, kunashuhudiwa sasa neema, kumejengwa kituo cha afya cha kisasa chenye vifaa tiba hata kuwaondolea adha wananchi, hasa wajazito kutembea kilometa 30 kwenda na kurudi hospitali ya manispaa hiyo, kutafuta huduma za afya ya uzazi na upasuaji.

Kabla ya kituo hicho, kata ilikuwa na zahanati iliyokuwa imeelemewa na wingi wa wagonjwa, kwa sababu vijiji zaidi ya vitano na kata jirani ya Mwanase iliyopo Msalala, kwa siku inahudumia wagonjwa 60 hadi 100, idadi ambayo ni kubwa kulinganisha uwezo wa kituo hicho.



.Mganga Mkuu wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama Dk. Josephat Shani (katikati) akitoa maelekezo ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kinaga kwa Mkuu wa mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (kulia) **PICHA; ZOTE: SHABAN NJIA.**

WAKAZI KINAGA;

Christina Nkuli mkazi wa kata ya Kinaga anasema, kabla ya kituo hicho walilazimika kutembea umbali wa kilometa 30 kwenda na kurudi hospitali ya kahama kutafuta huduma za afya ya uzazi na upasuaji, wengi walilazimika kujifungua majumbani kutokana na umbali huo na kuhatarisha usalama na vichanga vyao.

Anasema, ili kufika hospitali ya wilaya walilazimika kutumia usafiri wa pikipiki kwa gharama ya Sh. 10,000 mchana na usiku ikiwa ni Sh. 25,000 hadi 30,000 huku kwa gari mchana ikiwa ni Sh.70,000 na usiku ni Sh.120,000 hadi 150,000 na wale wasiokuwa na uwezo walikuwa wakihatarisha maisha yao kwa kujifungua majumbani.

"Hivi karibuni nilikuwa na mgonjwa mke wa mtoto wangu alikuwa na uchungu wa kujifungua na ulimpata majira ya saa nne usiku, nililazimika kukodi gari kwa Sh.70,000 na hii nililalamika sana kupunguziwa kwasababu wa gari alitaka Sh.120,000 nilimfikisha hospitali na alijifungua salama na sasa yupo nyumbani," aneleza Nkuli.

Katalima Mpuya anasema, kituo kimekamilika kwa hatua za awali na kuanza kutoa huduma kwa wananchi, hivyo wanaomba kiwe na gari maalumu la kubeba wagonjwa hasa wajawazito ili kuondokana na adha za kukodisha magari ya watu binafsi kwa gharama kubwa ili kuwanusuru wajawazito wasiokuwa na uwezo kuendelea kujifungulia majumbani kwa kushindwa kumudu gharama hizo.

**MGANGA MFAWIDHI**

Maria Julius, Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, anasema kituo kimejengwa kwa gaharama ya Sh. Milioni 569. 842 kati ya hizo Sh. Milioni 69.842 ni mapato ya ndani ya Halmashauri na kiasi cha Sh. Milioni 500 ni fedha kutoka serikali kuu na kimekamilika kwa asilimia 99 na kinatoa huduma.

Anasema, huduma zinazotolewa kwasasa ni wagonjwa wa nje (OPD) wazazi, matunzo na Tiba (VVU), kifua kikuu, Kiliniki ya baba, mama na mtoto, maabara na upasuaji na changamoto iliyopo ni kituo kutokuwa na huduma ya nishati ya umeme licha ya kuwepo kwa nguzo za umeme yapata miezi miwili sasa.

Vilevile anasema, kituo hicho kitawanufaisha wakazi 22, 342 wa kata ya kinaga na kitawaondolea adha ya kutembea umbali wa kilomета 30 kwenda na kurudi hospitali ya manispaa hiyo kutafuta huduma za afya ya uzazi na upasuaji sasa watakuwa wanazipata karibu tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

**ZAHANATI KUELEMEWA**

Julius anasema, zanahati iliyopo ilikuwa imeelemewa na wingi wa wagonjwa kwani kwa siku ilikuwa ikihudumiwa wagonjwa 60 hadi 100, kliniki maalumu wakihudhuria 100 hadi 150, wazazi 10 hadi 15 na wengi wa wagonjwa walikuwa wakitoka katika vijiji vya kinaga, Nduku, Mwagobeko, Mbilimbi na Kijiji cha Igung'hwa.

Anasema, huduma zinazotolewa zahanati ni pamoja na wagonjwa wa nje (OPD), wazazi, matunzo na tiba kwa wagonjwa wenye VVU, kifua kikuu(TB) pamoja na huduma za baba, mama na mtoto na wale waliotakiwa kupata huduma hospitali ya wilaya walilazimika kuwapatia rufani wakatibiwe zaidi.

Julius anasema, kufunguliwa kituo cha afya kutasaidia kutatua changamoto ya mrundikano wa wagonjwa kwani huduma za upasuaji, wazazi, wagonjwa wa nje (OPD), Kliniki ya baba, mama na mtoto, Kliniki ya matunzo na tiba, kifua kikuu, maabara na mionz i(X-Ray) zitapatikana karibu.

Diwani wa Kata hiyo Mary Manyambo, anasema, barabara inayotoka wilayani hadi katika kituo hicho ni mbovu hali inayosababisha wananchi kutumia pikipiki kwa gharama kubwa na kuiomba serikali kuingia kati na kuikarabati, ili kuiwezesha gari la kubeba wagonjwa kufika na kuchukua wagonjwa waliopewa rufani.

**KUTOJIFUNGUA VITUONI**

Mkazi wa Kijiji cha Nduku, John Kalugula anaeleza sababu ambazo zimekuwa zikisababisha wake zao kushindwa kujifungulia katika vituo vya afya ni kushindwa kuambiwa siku za makadirio ya kujifungua, wanapata uchungu na kuhangaika siku nzima na anakuja kutoa taarifa yuko hatua ya mwisho na ameshazidiwa.

Anasema, ili kuondokana na tatizo hilo wamejiwekea utaratibu wa kuhudhuria kliniki na wake zao ili kujua maendeleo ya watoto tumboni na kujua makadirio ya siku ya kujifungua ili kujiandaa wasiendelee kujifungulia majumbani, na wale wanaotakiwa kujifungulia hospitali za wilaya wawafikishe haraka ili kunusuru maisha yao.

Mganga Mfawidhi, Julius anaeleza sababu nne zinazowakwamisha wajawazito kushindwa kujifungua kituoni, ni pamoja na baadhi ya wenye umri zaidi ya miaka 35 waliobeba ujauzito kwa mara ya kwanza, wanajifungulia majumbani kwa kuogopa kupewa rufaani ya kwenda hospitali ya wilaya na badala yake wanajitokeza kliniki wakiwa na vichanga vyao mikononi.

Pia sababu nyingine ni wajawazito wanaojifungua kwa kufanyiwa upasuaji mara kwa mara, wanahudhuria kiliniki kipindi chote cha ujauzito lakini muda wa kujifungua hawaonekani na wanakuja kuonekana wakiwa na watoto jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao kwani baadhi huwa wanapata taarifa ya kupoteza uhai.

Pia, anataja sababu, wenye uzazi wa mimba nne na kuendelea na wanaopata ujauzito kwa mara ya kwanza na wanafanya hivyo baada ya kupewa elimu ya vidokezo vya hatari ambavyo wanaelimishwa kipindi wanachofika kuanza kiliniki ya kujua maendeleo ya mtoto tumboni.



Wakazi wa Kata ya Kinaga, Manispaa ya Kahama, wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Chiristina Mndeme (hayupo pichani) wakati wa hafla ya uzinduzi wa kituo cha Afya cha Kinaga.

**MKUU WA MKOA**

Christina Mndeme, Mkuu wa Mkoa Shinyanga, anasema, mkoa umepokea zaidi ya Sh. Bilioni 43 za huduma za afya, kati ya hizo Sh. Milioni 500, zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho.

Hapo anawataka wajawazito kuacha tabia ya kujifungulia majumbani kwani ni kuhatarisha maisha na vichanga vyao na badala yake wajifungulie kituo cha afya.

Anasema, serikali inasogeza huduma za afya kwa wananchi kwa kujenga vituo vya afya na zahanati, ikipambana na vifo vitokanavyo na uzazi kwa wajawazito na kuwataka pindi wanapopata ujauzito waanze kliniki haraka iwezekanavyo na sio kusubiria miezi isonge mbele ndipo waanze kliniki.

Mndeme anataja kuwapo maradhi mengi hivyo itakuwa sio vema mjamzito kujifungulia majumbani na kuzalishwa na mtu asiyekuwa na sifa ya ukunga au kukimbia kwa waganga wa jadi kwani kufanya, hivyo ni kuhatarisha maisha yao na vichanga vyao, na kuhakikisha wanafuata ushauri wanaopatiwa na watoa huduma hispitalini.

AFYA

# Kinababa wanavyotapeliwa biashara ya kuwapa ujauzito wahitaji India

**News Delhi, India**

Mapema mwezi uliopita Mangesh Kumarali kuwa akivinjari kwenye 'Facebook' alipokutana na video kutoka kwa "Huduma ya Ajira ya Wajawazito nchini India" na kuamua kuiangalia.

Kazi ilionekana nzuri.Bila shaka ni 'dili' nzuri sana kuwa kweli. Kufikia sasa, kijana huyo mwenye umri wa miaka 33, ambaye anapata rupia 15,000 ($180; £142) kwa mwezi akifanya kazi katika kampuni ya mapambo ya sherehe ya harusi, tayari amepoteza rupia 16,000 kwa walaghai - na wanaomba zaidi.

Mangesh, kutoka jimbo la kaskazini mwa India la Bihar, sio mtu pekee aliyeangukia kwenye mtego wa ulaghai huo.

Naibu Msimamizi wa polisi Kalyan Anand, anayeongoza kikosi cha kupambana na uhalifu wa mtandao katika wilaya ya Nawada ya Bihar, akasema kwamba kulikuwapo mamia ya waathiriwa wa ulaghai, wanaume walishawishiwa kutoa pesa zao kwa ahadi ya siku kubwa ya malipo na usiku katika hoteli , kumuwezesha mwanamke asiye na mtoto.



Walionaswa kutokana na kuhusika na biashara za ujauzito. **PICHA: MTANDAO.**

Hadi sasa polisi imewakamata wanaume wanane, kunasa simu tisa na mashine ya kuchapisha stakabadhi, bado wanawasaka wengine 18.

Lakini kupata walioathiriwa kunatajwa ni vigumu akinena: "Genge hilo limekuwa likifanya kazi kwa muda wa mwaka mmoja na tunaamini limewatapeli mamia ya watu, lakini hakuna hata mmoja ambaye hadi sasa amejitokeza kulalamika, labda kwa sababu ya aibu."

Pia, waathiriwa wawili - mmoja akasema amepoteza rupia 799. Mangesh anafichua zaidi kuwa baada ya simu kadhaa, akifichua jinsi alivyotekwa na matapeli.

"Dakika kumi baada ya kubofya video, simu yangu iliita. Mwanaume huyo aliniomba nilipe rupia 799 ikiwa ningetaka kujiandikisha kwa kazi hiyo," anasema.

Mpiga simu - Mangesh akamwambia kuwa atafanya kazi katika kampuni huko (mji) Mumbai na kwamba atakapojiandikisha, atatumiwa maelezo ya mwanamke ambaye angempa mimba.

Walimpa rupia nusu milioni - karibu mshahara wa miaka mitatu - ili tu kufanya mapenzi na mwanamke huyo na kuahidi zawadi zaidi ya rupia 800,000 ikiwa angepata mimba.

"Mimi ni maskini, nahitaji sana pesa kwa hiyo niliwaamini," baba wa watoto wawili wa kiume aliniambia.

Katika muda wa wiki kadhaa zilizofuata, Mangesh akatakiwa kulipia zaidi ya rupia 16,000 - rupia 2,550 ili kupata hati za mahakama, 4,500 kama amana ya usalama na rupia 7,998 kama Kodi ya Bidhaa na Huduma (GST) kwa pesa alizokuwa akienda kupata.

Amenishirikisha risiti zote na karatasi bandia za mahakama, hati inayoonekana rasmi ina jina lake na ina picha yake pamoja na ya mwanamume aliyevalia sare za polisi. Kwa herufi kubwa kubwa juu, inasema "Mkataba wa Kuzaliwa kwa Mtoto" na maandishi mazuri hapa chini yanasomeka "fomu ya uthibitishaji wa ujauzito".

Sahihi iliyo mwishoni mwa waraka huo inafanana na ile iliyotumiwa na mtangazaji wa kipindi cha mazungumzo cha Marekani Oprah Winfrey.

Walaghai hao walimvutia kwa kumtumia picha za wanawake saba, wakimtaka achague angependa yupi wa kumpa ujauzito.

"Walisema wangepanga chumba cha hoteli katika mji niliyokuwa nikiishi na nitakutana na mwanamke huyo huko," alisema.

Wakati Mangesh akiendelea kuuliza pesa alizoahidiwa, walimtumia risiti wakisema wameweka katika akaunti yake ya benki rupia 512,400, lakini pesa hizo zilikuwa zimesitishwa na zingelipwa baada ya kulipa shilingi 12,600 kama ushuru wa mapato.

Kufikia wakati huo, Mangesh anasema alikuwa amepoteza mshahara wa mwezi mzima na aliwaambia kwamba hawezi kulipa tena na akaomba kurejeshewa fedha.

"Lakini Sandeep Sir, akakataa na nilipokasirika, akaniambia kwa vile akaunti yangu ya benki ilionyesha mkopo wa rupia 500,000, mamlaka ya kodi ya mapato ingevamia nyumbani kwangu na kunikamata.

"Mimi ni mfanyakazi masikini, nilipoteza malipo ya mwezi mzima na sikutaka kujikuta katika kesi yoyote ya jinai. Niliogopa sana hadi nilizima simu yangu kwa siku 10. Niliiwasha tena siku chache zilizopita," akafafanua.

Kuna ufafanuzi, wanaume waliohusika na ulaghai huo ni wasomi na wanajua jinsi ya kufanya kazi kwa simu za rununu, kompyuta ndogo na vichapishaji.

Waathiriwa, kwa upande mwingine, wanatoka pande zote za India na wengi wao wana elimu ndogo.

Mangesh anasema, haikumshangaza kwamba huyu anaweza kuwa mdanganyifu kwa sababu "Sandeep sir" alikuwa amemtumia nakala za vitambulisho vyake, ikiwa ni pamoja na moja iliyomtambulisha kama askari wa jeshi la India.

'Pia aliamini kuwa picha iliyoonyeshwa kwenye 'Whatsapp' ya mpigaji simu - inayoonyesha mwanamke wa kigeni mwenye kuvutia akiwa amembeba mtoto mchanga mikononi mwake - ilikuwa ya kweli.

"Wewe niambie utakosa kuamini hiyo picha?" anauliza.

**KINACHOENDELEA**

Polisi wamewakamata wanaume wanane, kunasa simu tisa na printa, na wanawasaka wengine 18 ambao wametoroka.

Tatizo ni kwamba, mtaalamu wa sheria ya mtandao Pavan Duggal anaeleza: "Walaghai wiliwarubuni kwa ahadi ya pesa za bure na ngono bila malipo ambayo ni mchanganyiko hatari. Katika hali kama hizi, busara mara nyingi hupuuzwa'

Pamoja na ujio wa maradhi Covid-19 - wakati huduma ya benki kwa njia ya simu na mtandao ikawa jambo la kawaida, Duggal anasema "zama za uhalifu wa mtandao zilianza" na anaonya kwamba "itaendelea kwa miongo kadhaa".

Kadri wahalifu wa mtandao wanavyokuja na mbinu mpya zaidi, za kibunifu na zilizogeuzwa kukufaa zaidi, India italazimika kufanya kazi kwa bidii zaidi kulinda watu kama Mangesh dhidi ya kushambuliwa na walaghai," anaongeza, akiwa na ufafanuzi:

"Serikali pekee inatajwa haiwezi kufikia kila mmoja wa watu bilioni 1.4 wa India.Idadi ni kubwa mno. Kutegemea serikali pekee itachukua muda mrefu sana na uchumi wa India utaendelea kudhoofika. Kwa hiyo ni lazima serikali itoe motisha kwa sekta binafsi kujitokeza," anasema.

Inatajwa matapeli nao bado hawajakata tamaa, kama Mangesh anavyofafanua: "bibi" anapiga. Huyu, alinieleza baadaye, alikuwa mwanamke ambaye alikuwa ameahidiwa kukutana naye. Siku ya Jumapili usiku, aliniambia kuwa amekuwa akizungumza naye karibu kila siku.

"Nilimwambia sina pesa. Nilimsihi anirudishie pesa zangu, lakini akasema haitawezekana. Natamani angalau arudishe rupia 10,000," akainiambia.

"Kwa kweli sijui la kufanya sasa. Nimepoteza malipo ya mwezi mzima na sijaweza kutuma pesa zozote kwa familia yangu huko Bihar. Mke wangu ana hasira sana na hazungumzi nami," anasema, mtoa maoni.

"Wale walionidanganya lazima wapate adhabu ya juu zaidi. Ninafanya kazi ya ngumu ya kuvunja mgongo siku nzima kwa rupia 500. Najua nilifanya makosa makubwa. Lakini walichonifanyia ni makosa sana," anaeleza

**• Kwa mujibu wa BBC**



# HABARI DODOMA

## DC awataka wanafunzi waliofeli la saba kurudi darasani

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Mayeka Simon, amewataka wanafunzi waliofeli mtihani wa darasa la saba mwaka 2023 kurudia darasa hilo, ili kutimiza lengo la serikali ya kuifanya elimu ya kidato cha nne kuwa ya lazima.

Amesema ni suala la aibu kupoteza muda kujadili suala la wazazi kuwa kikwazo kwa watoto wao kupata elimu katika ulimwengu wa sasa na ameahidi kuishughulikia changamoto hiyo kikamilifu.

Aidha, aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kwa kuweka utaratibu maalumu wa kuwasaidia wanafunzi wasio na uwezo kwa kuwalipia gharama za masomo katika ngazi mbalimbali za kielimu kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vikuu.

Kadhalika aliagiza wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza kuhakikisha wanakwenda shuleni hata kama hawana sare za shule.

"Na wazazi kila mmoja ahakikishe anatoa ushirikiano wakutosha ikiwa ni pamoja na kupeleka chakula kwani kwa imani yake anaamini kuwa siri kubwa ya ufaulu wa mwanafunzi ni kupata chakula awapo shuleni.

"Hakuna kitu chochote kinachosaidia ufaulu kwa wanafunzi zaidi ya wanafunzi kupata chakula shuleni," alisema Mayeka.

Vile vile alisisitiza wazazi kuhakikisha watoto wao wanakwenda shuleni mapema iwezekanavyo ili kuendelea na masomo ya darasa la saba, kwani hatua kali zitachukuliwa kwa yeyote atakayepuuza agizo hilo.

Sambamba na agizo hilo aliwahimiza wazazi wote wenye wanafunzi shuleni kushirikiana na walimu kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuhakikisha wanafunzi hao wanapata chakula wanapokuwa shuleni kwani inasaidia kuinua kiwango cha ufaulu.

Ili kukomesha tabia ya watoto kuajiriwa kazi za ndani katika miji mbalimbali, Mayeka alitoa wito kwa jamii kutoa ushirikiano kuwafichua madalali wote wanaojihusisha na kushawishi watoto wenye umri wa kuwa shuleni kwenda kufanya kazi za ndani.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, White Zuberi, alipongeza agizo hilo ambalo limetokana na maazimio ya vikao vya kisheria vya halmashauri na kwamba uamuzi huo unalenga kuwakomboa wanafunzi hao.

Mkuu wa Divisheni ya Elimu Awali na Msingi, Margareth Temu, alisema wanafunzi 416 wa darasa la saba walifeli mtihani wa taifa mwaka jana.

Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai, alikemea tabia ya baadhi ya wazazi kuwashawishi watoto wao kujifelisha kwa malengo ya kuajiriwa kazi za ndani.

Hivyo aliwataka watoto hao kujitambua na kufahamu kwamba maisha yao ya baadaye yanategemea sana elimu yao.

## Mafuriko yabomoa nyumba 22 mkoani Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

NYUMBA 22 za wakazi wa Kijiji cha Mwankhalaja mkoani Singida zimebomoka kutokana na mvua inayoendelea kunyesha na kusababisha mafuriko. Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thomas Apson, akizungumza jana baada ya kutembelea kijiji hicho kilichokumbwa na mafuriko hayo yaliyotolea mwishoni mwa wiki alisema mafuriko hayo yamesababisha kaya 22 kukosa mahali pa kuishi. Aliwaambia waathirika wa mafuriko hayo kuwa serikali ipo pamoja nao na itahakikisha inawasaidia ambapo katika hatua ya kwanza imetoa maturubai kwa wananchi hao ambayo watayatumia kutengeneza mahema ya kuishi kwa muda.

Apson alitoa wito kwa wananchi walio karibu na majaruba ya mpunga kipindi hiki wahame maana ni rahisi kufikiwa na mafuriko na pia wasijenge nyumba zao katika eneo la majaruba ya mpunga.

Pia aliwatia moyo waathirika wa mafuriko hayo kwamba serikali itaendelea kuwasaidia kwa kuleta maturubai na mahema zaidi ambayo yatawasaidia katika kipindi hiki wakati wakisubiri kujenga nyumba zao.

Nao baadhi ya waathirika wa mafuriko hayo waliomba serikali na wasamaria wengine kuwasaidia misaada mbalimbali kwani mafuriko hayo yamesababisha wakose hata chakula kutokana na vyakula kusombwa na maji. Mmoja wa waathirika hao, John Hamneta alisema: "Kimsingi hali yetu ni ngumu hapa tulipo hatuna hata vyakula tunawaomba wasamaria wema watusaidie katika kipindi hiki ambacho tumepatwa na janga hili maana hata watoto wetu watashindwa kwenda shule".




Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. bilioni 3.4 kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, kwa ajili ya kulipa fidia ya ardhi kwa wananchi waliopitiwa na miundombinu ya serikali kwenye maeneo yao katika kata za jijini humo juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Madiwani waomba kushirikishwa ujenzi wa miradi ya umeme

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MADIWANI wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida wameliomba Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Singida linapotekeleza miradi yake liwe linawashirikisha madiwani wa maeneo husika, ili kutambua vijiji na vitongoji vyenye uhitaji wa huduma ya nishati ya umeme.

Walitoa ombi hilo juzi kwenye kikao cha wadau wa nishati ya umeme mkoani Singida kilichoandaliwa na shirika hilo na kuwashirikisha baadhi ya wakuu wa taasisi za serikali kwa lengo la kutangaza huduma wanazozitoa na kupokea maoni na changamoto mbalimbali.

Walisema endapo TANESCO itaweka utaratibu wa kuwashirikisha madiwani kutaondoa malalamiko ya wananchi ambao baadhi ya vijiji vyao bado havijafikishiwa huduma ya umeme.

Diwani wa Kata ya Kisaki, Moses Ikaku alitoa mfano wa Kitongoji cha Ilahu kuwa na umeme lakini TANESCO wakakitaja Kitongoji cha Ikenda kuwa ndicho chenye umeme badala ya Ilahu jambo ambalo linaweza kuwaletea wananchi usumbufu.

Aidha, madiwani hao waliziomba taasisi za umma mkoani hapa kushirikiana wakati wa utekelezaji wa miradi yao ili kuepusha migongano kama Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kuilalamikia TANESCO kuwa wameweka nguzo zao kwenye hifadhi ya barabara au Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA), wamepitisha mabomba ya maji kwenye miundombinu ya umeme.

Naye Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu, alizitaka taasisi zote za serikali mkoani Singida kuwa na uhusiano na mawasiliano.

Kiaratu alisema wamekuwa wakikutana na changamoto hizo wakati wa utekelezaji wa miradi mbalimbali na kuwa Manispaa ya Singida katika mpango wao wa kupanga mji walizishirikisha taasisi zote na kukubaliana lakini anashangaa wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo wanakwenda tofauti.

Alisema taasisi moja inapokuwa na mradi ni vizuri kabla ya kuuanza itoe taarifa kwa taasisi zingine ili kuondoa kadhia hiyo ambayo mara nyingi husababisha miundombinu iliyopo kubomolewa na kuisababishia hasara serikali.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Singida, Mhandisi Mwamvita Ally, alisema wamezipokea changamoto za madiwani hao na kuwa zitafanyiwa kazi ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma sahihi, bora na kwa wakati. Aidha Ally alisema ili kukabiliana na tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara shirika hilo linafanya maboresho kwa kubadilisha nguzo zilizooza na kuweka vikombe.

Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja wa shirika hilo, Mkoa wa Singida, Rehema Mwaipopo, akielezea utekelezaji wa miradi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mkoa wa Singida alisema shirika hilo kwa sasa inasimamia miradi miwili ya maendeleo.

Alisema mradi huo wa kupeleka umeme katika maeneo, vitongoji na mitaa iliyopo pembezoni mwa miji (vijiji-miji) yaani peri urban ambayo yanauhitaji mkubwa wa umeme lakini pia hali ya maeneo hayo inashabihiana na maeneo ya vijijini.





Baadhi ya vijana wakazi wa Mji Mdogo wa Mbalizi, mkoani Mbeya wakiondoa tope lililoziba moja ya mitaro na kusababisha maji kushindwa kupita na kujaa kwenye maduka na makazi ya watu katika mji huo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ludewa yang'ara kuripoti wanafunzi awali, la kwanza

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

HALI ya kuripoti kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na awali wilayani Ludewa mkoani Njombe ni ya kuridhisha, huku kwa upande wa kidato cha kwanza ikiwa ni ya kusuasua.

Hayo yalibainika wakati wa ziara ya Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Mathan Chalamila, iliyolenga kukagua mwenendo wa kuripoti kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza, darasa la kwanza na awali wilayani Ludewa.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo, Chalamila alisema ameridhishwa na mapokezi ya wanafunzi hao kwenye baadhi ya shule za msingi. Hata hivyo alitoa agizo kwa walimu na wazazi kuhakikisha wanafunzi wote wanaotakiwa kuanza kidato cha kwanza wanaripoti ndani ya wiki moja. "Hali ya wanafunzi kuripoti kwenye baadhi ya shule za sekondari bado ipo chini, hivyo niwasihi wazazi kuwapeleka watoto wao shuleni kwani kitu pekee ambacho kinaweza kumbadilisha mtoto ni elimu endapo itakuwa kinyume na hapo basi tutatengeneza kizazi cha baadaye ambacho hakitakuwa na uelewa na kuwa wazururaji mtaani," alisema Chalamila.

Naye Katibu Tawala Wilaya ya Ludewa, Gilbert Sandagila, alisema maandalizi ya shule ikiwamo vyumba vya madarasa yapo vizuri kwa kuwapokea wanafunzi hao, hivyo wazazi wahakikishe wanafunzi wote waliochaguliwa wanajiunga na shule kwa wakati.

"Serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imewekeza pesa nyingi kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule ili watoto waweze kupata elimu bora, hivyo niwasihi wazazi wote kuwapeleka watoto shule," alisema Sandagila. Kwa upande wake Kaimu Ofisa Elimu Sekondari, Munawale Swai, alisema Idara ya Elimu Sekondari imejipanga vizuri kwa ajili ya kuanza mwaka wa masomo.

"Walimu wapo, vyumba vya madarasa vipo vya kutosha sambamba na rasilimali za ufundishaji tunachosubiri ni wazazi kuleta watoto wao shuleni ili waweze kupata elimu," alisema Swai.

Swai alitaja moja ya sababu ya kuchelewa kuripoti kwa wanafunzi hao ni wazazi kutofanya maandalizi ya mahitaji ya watoto wao ya kutosha wakidai kuwa wanasubiri siku ya gulio ndipo wakanunue mahitaji.

# Mjimwema Njombe wahoji kukwama ujenzi wa shule

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wa Mtaa wa Ngalanga, Kata ya Mjimwema, mkoani Njombe, wameiomba serikali kuharakisha kwa ujenzi wa shule ya msingi katika eneo hilo, kwamba hivi sasa watoto wao wanatembea umbali mrefu kwenda shule iliyopo kata jirani.

Waliwasilisha ombi hilo jana wakati wa mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika ambapo mbali na kuomba kuanza kwa ujenzi wa shule hiyo haraka wengine wamelalamikia wingi wa michango shuleni hususani ya chakula ambayo inatofautiana na shule nyingine.

Hata hivyo wananchi hao wamechangishana zaidi ya shilingi milioni 14 ili kulipa fidia eneo itakapojengwa shule hiyo lakini bado hatua za ujenzi hazijaanza.

"Tunafikiria kwanini shule ya Ngalanga haijengwi, tutawapeleka wapi watoto wetu, shule ikijengwa hapa tutafurahi sana kwa sababu inakwenda kutatua changamoto ya watoto kutembea umbali mrefu hata sisi wazazi tunakosa amani," alisema Simon Katolo.

Naye Boniface Kivi alisema tayari wamechanga fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule na walichotarajia ni kuona kwamba serikali inawaunga mkono kwa haraka.

"Hizi hela tunazozichanga tulifikiri mbunge (Deo Mwanyika) umekuja kwa kusema kwamba tunaanza ujenzi wa shule uanze mara moja kwa sababu mambo ya ardhi umeshamaliza nayo ili tuwe na nguvu kwenye ujenzi sisi Wanangalanga," alisema Kivi.

Diwani wa Kata ya Mjimwema, Nestory Mahenge, alimwomba Mbunge wa Njombe Mjini kuwasaidia kupigania mchakato wa shule hiyo, kwani wakazi wake wanapata adha kubwa kwa kupeleka watoto mbali.

Kwa upande wake Mbunge Mwanyika alisema kwa kuwa anayo nafasi ya kupigania ili kuanza kwa ujenzi wa shule hiyo kwenye upande wa halmashauri pamoja na wadau.

Alisema" "Sisi tunachoangalia ni ujenzi wa shule, kuanzisha ujenzi pale mimi kama mbunge nitaongeza mchango wangu kwenye michango mliyotoa ili sasa ifike milioni 20 kamili sasa huu ndio mtaji wetu tunakwenda halmashauri ili tupate pesa," alisema Mwanyika.

# TANESCO yamaliza kero sugu ya umeme Makambako

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Makambako, limeanza kutatua changamoto ya umeme katika eneo la Juhudi Road liliopo Mtaa wa Kipagamo Halmashauri ya Mji wa Makambako Mkoa wa Njombe ambalo lilikuwa likilalamikiwa na wananchi kwa muda mrefu.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Meneja wa Tanesco Makambako, Alexnder Dumah alisema mpaka sasa zaidi ya nguzo 37 zimewekwa katika eneo hilo.

"Kweli kwenye eneo hilo kulikuwa na changamoto lakini tangu mwaka wa fedha huu umeanza, tumepata vifaa tumeweza kuwafikishia huduma wateja wetu na kinachoendelea ni kukamilisha kuweza kuwasha ili wananchi waweze kulipia ili kufungiwa mita," alisema Dumah.

Hata hivyo Dumah aliwataka wananchi wenye changamoto ya umeme kufika ofisini ili wawasilishe kero zao ziweze kutatuliwa.

Aliongeza kuwa wataendelea kuwafikishia wananchi huduma ya umeme katika maeneo yao kwa kadri fedha zitakavyopatikana huku akiwataka kutunza miundombinu hiyo.

"Tunamiradi mingi inaendelea, nawaomba wananchi hasa kwenye upande wa miundombinu mikubwa wawe makini sana kwenye muda kuchoma moto maana yake inasababisha nguzo kuungua na kusababisha kukosekana kwa umeme muda mrefu," alisema Dumah.

Diwani wa Kata ya Makambako, John Ngimbudzi, alikiri kuanza kuwekwa kwa nguzo na waya kufungwa katika eneo hilo na kueleza kuwa bado wananchi wengi wanauhitaji na huduma hiyo.

"Kuna unafuu kidogo lakini wananchi walio wengi bado hawajapata umeme, tunashukuru watu wa Tanesco kwa kutatua changamoto lakini bado," alisema Ngimbudzi.

Nao baadhi ya wananchi wa eneo hilo, Stanely Mbembati na Jeshi Sanga walisema licha ya nguzo kuanza kuweka na waya kufungwa bado baadhi yao hawajafikiwa na umeme na wameliomba shirika hilo kuona namna ya kuwafikishia huduma hiyo wananchi wote.

Alisema: "Kwa kweli juhudi zinaendelea wamesikia kilio chetu, tumekuwa tukilia muda mrefu lakini tunaomba wengi wetu bado tunauhitaji wa umeme kwa ajili ya kufanya shughuli za kimaendeleo".





# Ujenzi Bandari ya Maruhubi waiva, mkataba wasainiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar na kampuni ya Devco kutoka Uholanzi zimetiliana saini ya ujenzi wa Bandari ya Maruhubi.

Hafla hiyo utiaji saini wa mkataba huo ilishuhudiwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi katika viwanja vya Ikulu.

Katika shughuli hiyo, upande wa Zanzibar uliwakilishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Khadija Khamis na kwa kampuni ya Devco iliwakilishwa na Mtendaji Mkuu, Matthew Vander Borgh.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Mwinyi alisema bandari hiyo mpya ni fursa kubwa kibiashara, kiuchumi na kutoa huduma bora kwa wananchi. Aliwashukuru wote waliohusika ikiwamo Wizara ya Ujenzi, Shirika la Bandari, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Alisema serikali inasera ya kushirikiana na sekta binafsi na utiaji saini huo utakua ni ushirikiano mkubwa wa kwanza kutokana na ukubwa wa mradi huo.

Alisema hali ya Bandari ya Malindi siyo nzuri kutokana na kuwapo na msongamano wa abiria pamoja na usalama mdogo.

"Tumejipanga kuwa na usafiri wa umma wa mabasi unaotumia gesi na umeme ili kutunza mazingira, usafiri wa majini na usafiri wa boti za mwendo kasi," alisema.

Aliwataka wadau kutoa msaada ili ujenzi huo ukamilike kwa haraka na kuwataka kuondoa urasimu kwa wawekezaji.

Mkurugenzi wa Bandari Zanzibar (ZPC), Akif Muhammed, alisema bandari hiyo italeta mageuzi makubwa katika sekta ya usafirishaji na kuondosha changamoto za usafiri.

Alisema ujenzi wa mradi wa bandari kuu ya abiria utakua na awamu mbili ambapo awamu ya kwanza utagharimu Dola za Marekani milioni 250 na gharama zote za ujenzi Dola za Marekani milioni 400.

Alisema kwa mara ya kwanza Zanzibar itakua na usafiri wa ndege za baharini na kuirejesha historia ya Zanzibar kuwa kitovu kikuu cha biashara Afrika Mashariki.

Alisema ajira za muda 100 zitapatikana wakati ujenzi wa bandari hiyo ukiendelea na utakapokamilika kutakuwa na ajira za kudumu 600.

Aidha alisema bandari hiyo itakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 8,000 kwa siku na itakuwa chanzo kikuu cha uchumi na Zanzibar itabeba sifa ya kituo kikuu cha biashara.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akishuhudia Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Khadija Khamis Rajab kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi akitiliana saini makubaliano na Mkurugenzi Mkuu na Mwanzilishi wa Kampuni ya ZF Devco, Matthew Vander Borgh ya ujenzi wa Bandari mpya ya Maharubi Mpiga Duri Mkoa wa Mjini Magharibi itakayojengwa na kampuni hiyo ya nchini Uholanzi. **PICHA: IKULU**

# Balozi Karume apinga Katiba ya Zanzibar kurekebishwa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MTOTO wa Rais wa kwanza wa Zanzibar, Balozi Ali Karume, amepinga wazo la Katiba ya Zanzibar kufanyiwa mabadiliko na kuongezwa muda wa urais kutoka miaka mitano hadi saba.

Balozi Karume, alitoa msimamo wake alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jana nyumbani kwake Maisara Mkoa wa Mjini Magharib Unguja katika kuelekea maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi Zanzibar.

Alisema ni kosa kubwa kufikiria kufanya marekebisho ya Katiba kwa kumtazama mtu wakati mfumo uliopo wa kikatiba unajitosheleza kwa rais kukaa kwa muda wa miaka mitano.

Alisema mabadiliko yoyote ya Katiba ya Zanzibar yatakayofanyika yataleta mgongano katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa vile wabunge katika majimbo watalazimika na wao kuongezewa miaka saba badala ya mitano.

Alisema wabunge wanasimamiwa na Sheria ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuwa wakala wa uchaguzi kwa upande wa majimbo 50 ya Zanzibar.

Aidha alisema pia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani na wao watalazimika kuongezewa muda wa miaka saba jambo ambalo linamadhara makubwa na hakuna sababu za msingi za kufikiria jambo kama hilo.

"Kama leo utamwongezea muda rais aliyemadarakani, akaja na rais mwingine akataka kuongezewa muda zaidi ya huo, huwezi kumzuwia na tumeshuhudia wapo viongozi katika nchi jirani hawataki kuondoka madarakani baada ya kuondoa ukomo wa urais katika katiba zao," alisema.

Hata hivyo alisema haikuwa sahihi kwa kiongozi wa ngazi ya juu kutangaza hadharani kuwa watapeleka mapendekezo katika Sekretarieti ya Kamati Kuu ili Katiba ya Zanzibar ifanyiwe marekebisho kutoka miaka mitano hadi saba.

Mwishoni mwa wiki Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Mohammed Said Dimwa wakati akiweka jiwe la msingi katika Soko la Mwanakwerekwe alitoa pendekezo la kuongezewa muda wa uongozi Rais Mwinyi.

Dimwa alisema suala hilo halina mjadala na litafanyika bila rais kuulizwa kwa sababu ameonesha uwezo mkubwa wa kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar tangu kushika wadhifa huo.

# Makamu wa Rais ahimiza ajira kwa vijana wazalendo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni muhimu kwa taasisi zinazosimamia uwekezaji, uchumi na biashara kuweka kipaumbele suala la kutoa ajira kwa vijana wazalendo, hususani katika miradi ya maendeleo inayoanzishwa kwenye maeneo yao.

Aliyasema hayo juzi katika Kijiji cha Paje Mkoa wa Kusini Unguja, alipofungua mradi wa nyumba za makazi unaomilikiwa na raia wa Ujerumani.

Makamu huyo alisema haitokuwa jambo la busara kwa miradi ya uwekezaji na maendeleo inayoanzishwa nchini vijana kutopewa fursa.

Othman alisema kwamba hatua hiyo ni kuunga mkono jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana vyema ili kila kijana aweze kupata ustawi na kuwa na mazingira yatakayomuwezesha kuchangia maendeleo yake na taifa.

Alisema kwamba serikali katika kutimiza malengo ya mapinduzi ya mwaka 1964 ni pamoja na kukuza ustawi wa wananchi kwa kuwawezesha kuwa na njia ya kujipatia kipato ili kukimu mambo ya msingi katika maisha yao ya kila siku.

Aidha alisema kwamba sekta ya utalii inaendelea kupata mafanikio makubwa na kwamba serikali inaendelea kuvutia uwekezaji mkubwa kwenye sekta hiyo.

Alisema kwamba kuwepo kwa usalama na amani nchini ndiyo chachu ya kuwavutia wawekezaji zaidi ili uwekezaji uwe na tija kwenye nchi na kwamba katika kipindi cha miaka mitatu Zanzibar imetekeleza miradi mingi ya uwekezaji.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar, Shariff Ali sheriff, alisema sekta ya uwekezaji inazidi kupata mafanikio makubwa na kwamba taasisi hiyo imefanikiwa kuleta mradi mkubwa wa hoteli yenye nyota saba inayojengwa eneo la Vumawimbi kisiwani Pemba.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema mkoa huo umebahatika kuwa na ardhi kubwa kuliko mikoa yote ya Zanzibar na kwamba unanafasi kubwa katika kuendeleza miradi mikubwa ya kibiashara kwa maendeleo ya Zanzibar.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema serikali ipo bega kwa bega na wekezaji na itandelea kuwakilishia shughuli zao kuwa salama.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya CPS inayomiliki mradi huo, Tobias Diehold alisema huo ni mradi wa kwanza Zanzibar ambao unatumia teknolojia ya kisasa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAFIDH HAIDARY BAITAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3881/0026 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia AHMES SEKONDARI mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/26055/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GLORY ELIETI SAIDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S 2686/0016 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia kupitia KWANGU SECONDARY SCHOOL mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/TEM/4103/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAILES DOMINICUS MWANUKE**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA MITSUBISHI CANTER YENYE NAMBA ZA USAJILI T 413 AXX YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI
**TAARIFA PHQ/IRI/IRI/487/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JASVEER SINGH SOHAL**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA SCANIA R143 RANGI NYEUPE YENYE USAJILI T 210 CWT YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI
**TAARIFA PHQ/IRI/IRI/488/2024**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya CHAMWINO MJINI**
**Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO**
**Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na 107/2023**
**Jina la ALLY SALUMU.........MDAI**
**Jina la SHAKIRA SHILA............MDAIWA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo )**

**Kwa SHAKIRA SHILA DODOMA**
Kwa kuwa Mdai/ Wadai ameleta/ Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai ) TARAKA NA MGAWANYO WA MALI
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 16 Mwezi 01 Mwaka 2024 saa 2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 09 Mwezi 01 Mwaka 2024

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Shauri la madai Na. 135/2023**
**Jina la Mdai ..... NYAMTODO WANJARA**
**Jina la Mdaiwa ..... ALPHONCE BONIPHACE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya (18) ya Kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA: ALPHONCE BONIFACE NG'HONG'HONA**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TALAKA KUACHANA MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 25 mwezi 01 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinanyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 04 Mwezi 01 Mwaka 2024.

HAKIMU
PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 372 of 2024**
**In the matter of the estate of the late GODWIN HERMAN SHEMBILU of Sombo within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by HELIME SINGANO**
**GENERAL CITATION**
**Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 12 day of 2...................... 2024
Dated at Dodoma this 09 day of 01................2024

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,
KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mahakama yathibitisha ushindi wa Tshidekedi

**KINSHASA, DRC**

MAHAKAMA ya Kikatiba nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imemthibitisha rasmi Rais Félix Tshisekedi Tshilombo, kuwa mshindi katika uchaguzi wa urais uliyofanyika Desemba 20, mwaka jana.

Rais Tshisekedi amepata zaidi ya asilimia 73 ya kura zote.

Mahakama hiyo ilikataa maombi ya kufuta matokeo hayo na kuitisha uchaguzi mwingine yaliyopelekwa na mgombea mmoja wa upinzani.

Kulingana na matokeo ya mwisho yaliyotangazwa na mahakama hiyo, rais anayemaliza muda wake ameongezewa kura kwa kuwa na asilimia 73.47, tofauti na ile ya awali iliyotangazwa na Tume ya Uchaguzi (CENI) ambayo ilimpa asilimia 73.34.

Mahakama hiyo ya katiba iliondoa kura za wagombea 26 wa urais ambazo zilizorekodiwa katika majimbo mawili ambapo CENI ilifuta matokeo kutokana na kuwepo na udanganyifu mbalimbali.

Awali Januari 5, CENI ilifuta kura kwa wagombea wengine 82.

Uchaguzi Mkuu uliofanyika Desemba 20, ulijumuisha nafasi ya urais, wabunge kitaifa na mikoa pamoja na madiwani.

Takwimu za mwisho zilizoanishwa na Mahakama hiyo haibadilishi orodha ya wagombea 26 ambao walikuwa kwenye kinyang'anyiro cha urais, lakini hubadilisha kidogo asilimia ya kura zao walizopata.

Katika matoke ohayo, mshindi Félix Tshisekedi anafuatiwa kwa mbali na gavana wa zamani wa Katanga Moise Katumbi, ambaye alipata asilimia 18.08 matokeo hambayo mahakama haikubadilisha na alama za mshindi wa tatu Martin Fayulu, ilipunguzwa hadi asilimia 4.92 kutoka ile ya awali 5 .33.

Mgombea mwingine, Waziri Mkuu wa zamani Adolphe Muzito, aliongezewa alama moja ya asilimia 1.13 kutoka 1.12.

Mahakama hiyo ya kikatiba ilichunguza ombi la mgombea mmoja wa upinzani, ambaye alishika nafasi ya mwisho akidai kufutwa kwa uchaguzi wa urais uliogubikwa na kasoro nyingi.

Baada ya kupitia maombi hayo, mahakama hiyo ilikataa ombi hilo na kutaka taratibu zingine ziendelee.

**RFI**



Wanajeshi wa Ecuador wakifanya doria nje ya kituo cha TV ambacho juzi kilivamiwa na waasi na kuwaweka mateka watangazaji. **PICHA: MTANDAO**

## Marekani, Uingereza kulinda meli katika bahari nyekundu

**LONDON, Uingereza**

VIKOSI vya jeshi la majini kutoka nchi za Uingereza na Marekani vimezuia shambulizi kubwa zaidi kuwahi kufanywa na waasi wa Houthi wa nchini Yemen, ikizilenga meli zinazopita katika bahari Nyekundu.

Taarifa kutoka Wizara ya Ulinzi ya Uingereza ilisema kundi hilo linaloungwa mkono na Iran lilirusha ndege 18 zisizo na rubani na makombora matatu juzi usiku na kuharibiwa na vikosi hivyo.

"Ndege na makomboya yaliangushwa kupitia mitambo iliyofungwa katika meli nne za kivita.Hakuna majeraha au uharibifu ulioripotiwa," ilisema taarifa hiyo.

Wahouthi hawajajibu chochote kuhusu mashambulizi hayo, ambayo yanalenga meli za wafanyabiashara ili kutoa shinikizo la kusitishwa kwa vita inayoendelea Ukanda wa Gaza.

Jeshi la Marekani lilisema shambulio la Jumanne lilikuwa la 26 tangu Novemba 19, mwaka jana.

Marekani, Uingereza, Ujerumani, Italia, Australia na Japan zimeonya kundi la Houthis kukomesha mara moja mashambulizi ambayo walisema ni kinyume cha sheria na ni tishio la moja kwa moja kwa uhuru wa usafiri katika njia hiyo bahari inayopitisha asilimia 15 za meli za biashara.

Nchi hizo washirika wamepinga mashambulizi hayo yanayofanywa na waasi hao kaskazini-magharibi mwa Yemen kama njia ya kulipiza kisasi.

Waziri wa Ulinzi wa Uingereza, Grant Shapps alionya kwamba ikiwa mashambulizi yataendelea kundi hilo libeba mzigo wa lawama.

"Tutachukua hatua zinazohitajika kulinda maisha ya watu wasio na hatia na uchumi wa dunia," alisema Waziri Shapps.

## Rais Ruto amchokonoa tena Kenyatta

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Kenya, William Ruto, ametoa madai kwa utawala wa mtangulizi wake, Uhuru Kenyatta, kuwa ulitenga bajeti maalumu kwa ajili ya kuwahonga maofisa wa idara ya mahakama ili kutoa ushawishi kimaamuzi.

Akizungumza wakati wa kuweka jiwe la msingi katika mradi wa nyumba za bei nafuu ulioko Kapsuswa katika Kaunti ya Uasin Gishu, Rais Ruto, kwa upande wake hataogopa wala kutrtrrela azma yake ya kukomesha ufisadi ndani ya maakama.

Aliiwakemea watu wanaokosoa mradi huo wa majaribio akisisitiza hatakatishwa tamaa katika kazi zake za kuwakomboa Wakenya.

Hayo yanajiri wiki moja baada ya nyumba za wakazi wa mtaa wa Pioneer kubomolewa katika eneo hilo kwa lengo la kujengwa kwa nyumba za bei nafuu. Wakazi hao walidai kuwa hawakupewa taarifa kuhusu mradi huo.

Rais Ruto aliwahi kuwa mjumbe wa eneo hilo kwa miaka kumi.

Alisema serikali yake haitatenga bajeti ya kuwahonga maofisa wa idara ya mahakama.

"Watu fulani wanasema kwamba kwa sababu serikali iliyopita ilikuwa na bajeti ya kuwahonga mahakama, hivyo na mimi niweke bajeti ya kuwahonga watu wa mahakama. Je, mnataka pesa yenu itumike kuhonga mahakama? Aliwahoji wananchi waliohudhuria shughuli hiyo na kisha alisisitiza "Hakuna bajeti itakayotengenezwa kumhonga yeyote mahakamani. Mahakama ni ya watumishi wa Wakenya."

Kiongozi huyo ambaye alionekana kuwa na hasira, alirudia kauli yake kuwa kuna baadhi ya watu wanashirikiana na majaji kuvuruga miradi ya Kenya, ukiwamo mradi huo wa nyumba za bei nafuu.

Aliwahakikishia wakazi wa eneo hilo kwamba atapambana na ufisadi katika idara ya mahakama, na kwamba hakuna mtu atakayekuwa na ruhusa ya kuondoa ajenda iliyopangwa kwa ajili ya Wakenya.

Katika mradi huo, serikali itajenga nyumba 20000 katika mji wa Eldoret pekee.

**DW**

# Museveni akataa biashara zenye masharti

**KAMPALA, Uganda**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, amesema nchi yake itaendelea kufanya biashara na mataifa mengine ya kigeni ambayo hayaingilii uhuru wake wa ndani.

Kauli hiyo ya Rais Museveni, ameitoa siku chache tangu Marekani itangaze kuiondoa Uganda katika mkataba wa kibiashara AGOA.

Tangu atie saini na kisha kuwa sharia kamili ya ushoga, kiongozi huyo amekuwa katika shinikizo kutoka kwa mataifa ya magharibi yanayotaka abatilishe sharia hiyo, ambayo wanasema inakiuka haki za binadamu.

Marekani ilitishia kwa mara ya kwanza kuiwekea vikwazo Uganda na kuiondoa kutoka kwa mkataba wa biashara wa AGOA mwezi Mei mwaka jana, baada ya nchi hiyo kupitisha sheria hiyo.

Sheria hiyo inatoa adhabu ya kifo kwa watu watakaothibitika kujihusisha na vitendo vya mapenzi ya jinsia moja.

"Kwa sasa, wale wanaotuwekea shinikizo, wanapoteza muda wao. Hatupaswi kuwa na wasiwasi kuhusu hilo," alisema Rais Museveni katika hotuba yake kwa taifa aliyoitoa juzi.

Katika hatua nyingine Rais Museveni, katika hotuba yake hiyo kwa ajili ya kukaribisha mwaka mpya, alionya kundi la waasi la ADF lenye makazi yake nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kwamba hawana nafasi ya kuendelea kufanya mauaji ndani ya nchi hiyo.

"ADF hawana nafasi ya kufaulu, tumewaangamiza wote kwa awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu na sasa tuko kwa awamu ya nne." Aliongeza Rais Museveni.

**RFI**

# MAXIME: IHEFU ITAFANYA VIZURI MZUNGUKO WA PILI

**Na Saada Akida**

SIKU chache baada ya kujiunga na timu ya Ihefu FC, Kocha Mecky Maxime amekiangalia kikosi chake na kusema timu hiyo ina uwezo wa kufanya vizuri katika mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Maxime amesema kama atapata ushirikiano mkubwa kutoka kwa uongozi wa timu hiyo na wachezaji kujituma zaidi ana uhakika wa kupata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yao na kuweza kujikwamua kutoka kwenye nafasi ya chini waliopo sasa kwenye msimamo wa ligi.

Akizungumza na Nipashe jana, Maxime alisema ameiona timu yake ina kwa sasa anafanya maboresho katika nafasi chache ili kutengeneza kikosi bora chenye kusaka ushindi katika michezo yake.

"Hatuwezi kujiondoa kwenye nafasi ya chini kama hatutakuwa na ushirikiano mzuri na wachezaji kupambana kutafuta alama tatu katika kila mechi zilizopo mbele yetu, kila mmoja wetu anatakiwa kujitoa katika mechi ili kupata matokeo mazuri mechi zetu zijazo," alisema kocha Maxime.

Aliongeza kuwa baada ya kukabidhiwa timu ameanza programu ya mazoezi kwa kuweka falsafa zake hasa katika kipindi hiki ambacho Ligi Kuu imesimama kwa muda kupisha michuano ya Afcon inayotarajia kuanza Jumamosi nchini Ivory Coast.

Alisisitiza hakutaka kuwapa muda wa kupumzika wachezaji wake kwa sababu anahitaji kupata muda wa kukaa na timu na kuanza kuingiza mifumo yake ili kikisuka kikosi chake kwa ajili ya duru la pili la Ligi hiyo.

Ihefu FC tayari imeshacheza mechi 14 za duru la kwanza imeshinda mechi tatu, imetoka sare mechi nne na wamepoteza michezo saba, wamekusanya pointi 13 wakishika nafasi ya 13 kwenye msimamo.



Wachezaji na viongozi wa Timu ya Mlandege wakishangilia juzi usiku kutinga hatua ya fainali ya michuano ya Kombe la Mapinduzi baada ya kuifunga APR kwa mikwaju ya penalti 4-2. Timu hizo hazikufungana kwenye muda wa kawaida. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfungaji bora Ligi Kuu aibukia Mashujaa FC

**Na Adam Fungamwango**

MFUNGAJI bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ya 2016/17, Abdurahman Mussa amesajiliwa na klabu ya Mashujaa FC siku chache kabla ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo inasema kuwa wamemsajili mchezaji huyo kwa ajili ya kuongeza nguvu katika nafasi ya ushambuliaji.

Klabu hiyo imesema hivi sasa ipo kwenye maboresho katika kipindi hiki ili kuhakikisha si tu kwamba inabaki Ligi Kuu, lakini pia kuwapa burudani mashabiki wa soka Kigoma.

Kocha Mkuu Mohamed Abdallah 'Bares,' amesema anaamini usajili anaofanya kwa sasa utakuwa na tija na kuifanya timu hiyo kuwa bora zaidi.

"Tunasajili maeneo ambayo tunaona kuna mapungufu, naamini usajili ni mzuri na tutakuwa na timu imara," alisema Bares.

Abdurahman alikuwa mchezaji wa Ruvu Shooting ambayo kwa sasa inaitwa JKT Tanzania na alishawahi kuwa mfungaji bora msimu wa 2016/17 akiwa sawa na Simon Msuva, wote wakipachika mabao 14.

Wakati huo Msuva alikuwa kwenye klabu ya Yanga kabla ya kwenda kucheza soka la kulipwa nchini Morocco kwenye klabu ya Difaa El Jadida mara baada ya ligi ya msimu huo kumalizika katika.

Mashujaa imeshafanya usajili wa wachezaji kadhaa kipindi hiki cha dirisha dogo, ikiwa tayari imeshawasainisha wachezaji, Emmanuel Mtumbuka kutoka Stand United ambaye ni mshambuliaji, winga Nyeyezi Juma kutoka Inter Star ya Burundi pamoja na kiungo Balama Mapinduzi kutoka Coastal Union.

## Ligi Wavu Dar kuanza Februari 10

**Na Shufaa Lyimo**

LIGI ya mpira wa wavu mkoa wa Dar es Salaam inatarajiwa kuanza kutimua vumbi Februari 10 mwaka huu kwenye viwanja mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Chama cha Mchezo huo Mkoa wa Dar es Salaam (DAREVA), Fredy Mshangama, alisema ligi hiyo itashirikisha timu 25 ambapo kati ya hizo timu 13 ni za wanawake na 12 ni za wanaume.

"Maandalizi yanaendelea vema kuelekea kwenye Ligi hiyo ambayo ninaamini itakuwa na upinzani mkubwa kwani kila timu inataka kuchukua ubingwa na hata maandalizi yao yanahakisi kutaka mafanikio," alisema Mshangama.

Aidha, alizitaja baadhi ya timu ambazo tayari zimethibitisha kushirki Ligi hiyo kuwa kwa upande wa wanaume ni Prisons, Jeshi Stars, JKT, Chui, High Voltage, Nyika, KIUT, TBS, Wazo, Kigamboni, Bandari, pamoja na Twalipo.

Kwa upande wa wanawake alizitaja timu hizo kuwa ni pamoja na Jeshi Stars, JKT, Chui, KIUT, Star girls, winnie Queens, Wazo, Tai, Dar City na Twalipo.

Mwenyekiti huyo ameomba makampuni na taasisi mbalimbali kujitokeza kudhamini mashindano hayo na kuziunga mkono timu hizo.

## Judo taifa wajifua kwa mashindano ya Afrika

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha wachezaji 12 cha Timu ya Taifa ya mchezo wa Judo kinaendelea kufanya mazoezi kwa ajili kushiriki mashindano ya Afrika ya 'All African Games' yatakayoanza Machi nchini Ghana.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha wa timu hiyo, Zaid Hamis alisema kwa sasa kikosi hicho kinafanya mazoezi mepesi katika viwanja vya Ukonga Dar es Salaam.

"Timu yetu inaendelea kujiimarisha huku tukisubiri siku ambayo itaiwekwa kambini na Serikali kwa kuwa ni jukumu lake, alisema Hamis.

Alisema baada ya Serikali kuingiza kambini timu hiyo benchi la ufundi watalazimika kufanya mchujo na kubakiza wachezaji saba pekee wenye uwezo na watakaokidhi vigezo vya ushiriki wa mashindano hayo ya kimataifa.

Aliongeza kuwa miongoni mwa wachezaji waliopo sasa kwenye timu hiyo wapo wachezaji watatu kutoka Zanzibar ambao wameungana na wa Tanzania Bara kuunda timu hiyo ya taifa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**AL-ETTIFAQ HAITASHINIKIZWA**

KLABU ya Al-Ettifaq haitashinikizwa kumuuza Jordan Henderson mwezi huu au kumruhusu kuondoka kwa mkopo, huku nahodha huyo wa zamani wa Liverpool akiwa na mazungumzo na kocha, Steven Gerrard na Mkurugenzi wa Michezo, Mark Allen **(Talksport)**

**SANCHO ATUA DORTMUND**

WINGA Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23 anatazamiwa kujiunga na Borussia Dortmund kwa mkopo, lakini atarejea katika klabu yake ya Manchester United baada ya kuitumikia kwa sababu klabu hiyo ya Ujerumani haiwezi kumudu kufanya mkataba huo kuwa wa kudumu.**(Mirror)**

**DRAGUSIN KUAMUA**

KLABU ya Bayern Munich imewasilisha ombi la kuchelewa kumnunua mchezaji anayelengwa na Tottenham Hotspur, Radu Dragusin na sasa utakuwa uamuzi wa beki huyo wa Genoa na Romania mwenye umri wa miaka 21 kuamua ni wapi anataka kuhamia. **(Sky Sports)**

**MBAPPE KUBAKIZWA**

RAIS wa PSG, Nasser Al-Khelaifi amesema anataka mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 25, ambaye mkataba wake unamalizika msimu wa joto, kubakia na mabingwa hao wa Ufaransa kwa kuwa ndio klabu bora kwake. **(RMC Sport)**

**KIMMICH AWANIWA PSG**

PSG inashughulikia mpango wa kumsajili kiungo wa kati wa Ujerumani, Joshua Kimmich mwenye umri wa miaka 28 kutoka Bayern Munich mwezi huu Januari. **(Sky Germany)**

**BRUNO KUBAKIZWA**

KLABU ya Newcastle United itakataa ofa yoyote ya Januari kutoka kwa PSG kwa kiungo wa kati wa Brazil, Bruno Guimaraes huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 akitua Tyneside. **(The i)**

**PALMER ALITAKA KUHAMA**

MSHAMBULIAJI wa England, Cole Palmer mwenye umri wa miaka 21 amesema alitaka kuhama kwa mkopo kutoka Manchester City msimu uliopita, lakini akaambiwa anaweza „kusalia au auzwe" kabla ya kujiunga na Chelsea. **(Sky Sports)**

**PAVLIDIS AFUATILIWA**

KLABU ya Fulham inamfuatilia mshambuliaji wa AZ Alkmaar na Ugiriki, Vangelis Pavlidis mwenye umri wa miaka 25, ambaye amekuwa akitazamwa na Chelsea, AC Milan na Barcelona wiki za hivi karibuni. **(Evening Standard)**

**SENSI ATAKIWA LEICESTER**

KOCHA wa Leicester City, Enzo Maresca anashinikiza kumnunua kiungo wa kati wa Italia, Stefano Sensi mwenye umri wa miaka 28 kutoka Inter Milan. **(Sky Sports)**

**FELIX MAMBO MAGUMU**

BARCELONA imesitisha mazungumzo kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Atletico Madrid anayecheza kwa mkopo Joao Felix, huku klabu hiyo ya Hispania ikiwa na mashaka kuhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 24 kwa sababu ya kushuka kiwango chake. **(Sport)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HENDERSON AWA LULU LIGI ZA ULAYA

●●● Timu za England, Ujerumani zakimbizana sokoni kuwania saini yake baada ya kutaka....

**LONDON, England**

AJAX ina nia ya kumsajili Jordan Henderson kutoka Al Ettifaq, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka klabu za Ligi Kuu England, EPL na Ujerumani kuwania saini ya kiungo huyo, kwa mujibu wa ripoti ya ESPN.

Nahodha huyo wa zamani wa Liverpool, Henderson, ambaye aliondoka Anfield msimu uliopita wa joto, ameripotiwa kutaka kurejea Ligi Kuu ya England ikiwa ni miezi michache tu baada ya kuhamia Saudi Arabia kama sehemu ya uhamisho.

Mshahara wa Henderson unaweza kuwa kikwazo kwa Ajax, chanzo kiliiambia ESPN, lakini wanaona uzoefu na nafasi ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 33 kama sehemu wanazohitaji kuimarisha.

Ajax ipo katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, baada ya kupata ahueni kutoka kuwa na mwanzo mbaya wa msimu.

Klabu mbili za Ligi Kuu England na timu moja kutoka Bundesliga pia zina nia ya kumsajili Henderson, vyanzo vilisema.

Henderson aliunganishwa na mchezaji mwenzake wa zamani wa Liverpool, Steven Gerrard huko Al Ettifaq Julai 2023 baada ya kumaliza kukaa kwa miaka 12 pale Anfield na kumfanya kushinda Ligi kuu, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la FA, UEFA Super Cup na Kombe la Klabu bingwa ya dunia.

Habari za kutaka kuondoka kwa Henderson zimekuja kama kikwazo kipya kwa Gerrard ambaye hivi karibuni alitaka kuimarishwa kwa kikosi chake wakati wa dirisha la usajili la Januari.

Gerrard pia amemuona msaidizi wake Ian Foster akiondoka kwenda kuchukua nafasi ya kocha katika klabu ya Plymouth Argyle mapema mwezi huu.

Al Ettifaq iko katika nafasi ya nane kwenye Ligi ya Saudia, pointi 28 nyuma ya viongozi Al Hilal na bila ushindi wowote katika michezo nane ya ligi iliyoanza Oktoba 28, 2023.

# RAIS WA PSG AKOMAA KUMBAKIZA MBAPPE

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa Paris Saint-Germain, Nasser Al-Khelaifi, amethibitisha kuwa anataka Kylian Mbappe kubakia kwenye klabu hiyo zaidi ya msimu huu wa joto.

Mbappe ameingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake na yuko huru kwa mara nyingine tena kuzungumza na klabu yoyote, huku Real Madrid wakiongoza kwenye mbio za kuwania saini ya Mfaransa huyo.

Ripoti zinazodai Mbappe tayari amekubali kujiunga na Madrid zilikanushwa hivi majuzi na wawakilishi wa mshambuliaji huyo, hata hivyo, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 akithibitisha hadharani kuwa bado hajafikia uamuzi.

Al-Khelaifi sasa ameapa kuendeleza pambano la kumbakiza Mbappe, akisisitiza kuwa angefurahi zaidi ikiwa atabaki Paris.

„Bila shaka nataka Kylian abaki, hilo ni la uhakika," alisema Al-Khelaifi akiwaambia waandishi wa habari.

„Yeye ndiye mchezaji bora zaidi duniani, na klabu bora zaidi kwa Kylian ni PSG. Yeye ndiye yupo katikati ya kila kitu."

Wakati PSG wakiwa na matumaini ya kumbakisha Mbappe, wababe hao wa Ufaransa hawajali uwezekano wa kumpoteza kwa uhamisho wa bila malipo baada ya makubaliano na Mbappe majira ya joto yaliyopita ambayo yanalinda fedha zao.

Mbappe ametia saini makubaliano ya kisheria ambayo yatamfanya arejeshe hadi euro milioni 80 iwapo ataondoka msimu huu wa joto, huku pia akiachana na baadhi ya bonasi ya uaminifu mwaka jana ambayo itarudishwa kwake tu ikiwa atasaini nyongeza ya mkataba.

Mkataba wowote mpya unaweza kutekelezwa hadi 2025, ingawa upanuzi wa muda mrefu ambao utazingatia kuwezesha uhamisho wa siku zijazo pia ni uwezekano.

Wakati huo huo, Madrid inasalia kuwa na nia ya kupata saini ya Mbappe, baada ya kukosa mwaka 2022 aliposaini nyongeza ya ghafla huko Paris.




# Klopp amlilia gwiji Beckenbauer

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Juergen Klopp ametoa neno juu ya gwiji wa Ujerumani, Franz Beckenbauer aliyefariki, akisema ndiye aliyechangia kukua kwa uchezaji wake wa soka.

Beckenbauer, ambaye aliongoza Ujerumani kushinda Kombe la Dunia mwaka 1974 na kushinda tena kama kocha mwaka wa 1990, alifariki Jumapili akiwa na umri wa miaka 78.

„Sitaki kuonekana kama rekodi iliyovunjwa, lakini ulimwengu wangu ungekuwa tofauti bila yeye," alisema Klopp kupitia tovuti ya klabu.

„Nilipata fursa ya kumfahamu vyema zaidi katika Kombe la Dunia mwaka 2006 na tayari mwaka wa 2005 kwenye Kombe la Shirikisho.

„Jinsi alivyofanya, mwenye moyo mwepesi, mwenye urafiki, mcheshi, mwenye umakini katika wakati unaofaa, hii ilikuwa ya kutia moyo sana. Hakuwahi kujifanya kuwa bora kuliko alivyokuwa, alijua kila mara kwamba alihitaji msaada, hasa kama kocha," alisema Klopp.

Klopp alisema hakuweza kuzungumza na vyombo vya habari vya Ujerumani siku ya Jumatatu kwani alihitaji muda kushughulikia kifo cha Beckenbauer kwani alikuwa na jukumu kubwa katika maisha yake.

„Alinifundisha kitu ambacho sikujua wakati huo nitakihitaji maishani mwangu, kwamba unaweza kuwa maarufu, unaweza kuwa mwingi kwenye media, kila mtu anazungumza juu yako na bado unaweza kuwa wewe mwenyewe," aliongeza Klopp.

Kocha huyo pia alikumbuka mazungumzo yake ya kibinafsi na Beckenbauer na mkewe Heidi wakati wa sherehe za kumbukumbu ya kuzaliwa kwake akitimiza umri wa miaka 75 na kuongeza kuwa alizungumza mara kwa mara na Beckenbauer na familia yake wakati wa ugonjwa wake.

„Miezi michache iliyopita tulipigiwa simu na alikuwa sawa, lakini niligundua kuwa hakuwa katika hali ya kawaida sana."

# Alexander-Arnold nje kwa wiki chache

**LIVERPOOL, England**

KOCHA Msaidizi wa Liverpool, Pep Lijnders, amethibitisha kuwa Trent Alexander-Arnold atakuwa nje ya uwanja kwa „wiki chache" kutokana na jeraha la goti alilolipata wakati wa ushindi kwenye mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Arsenal, Jumapili.

Alexander-Arnold alikuwa katika kiwango kizuri dhidi ya Washikabunduki hao, huku pasi yake ikipelekea Jakub Kiwior kujifunga mwenyewe kwenye Uwanja wa Emirates.

Akizungumza kabla ya mechi ya mkondo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Fulham Jumatano, Lijnders alifichua kwamba Alexander-Arnold alipata jeraha katika ushindi huo.

„Kwanza kabisa, baadhi ya habari zisizokuwa nzuri, Trent aliumia goti lake wakati wa mchezo uliopita," alisema Lijnders.

"Kwa hiyo amepasuka kidogo kwenye mshipa wa goti na atahitaji muda kupona, atakuwa nje kwa wiki kadhaa, ngoja tuone baada ya hapo.

„Atapumzika na tunatumaini atarudi pale alipokuwa. Kwa sababu kijana huyu alikuwa na uamuzi katika michezo yote na ndiye aliyetutengenezea nafasi mara kwa mara na kuipa timu unyumbufu wa hali ya juu," alisema Lijnders.

Kuumia kwa Alexander-Arnold kutakuwa pigo kubwa kwa timu ya Jurgen Klopp, ambayo imeegemea uwezo wake wa kuamuru kucheza kutoka kwa beki wa pembeni na nafasi ya kiungo wa kati msimu huu.

Kwa kukosekana kwake, chipukizi Conor Bradley anaweza kupewa nafasi zaidi baada ya kuvutia wakati wa kipindi cha pili mwishoni mwa wiki.

Katika habari njema zaidi kwa mashabiki wa Liverpool, Lijnders pia alifichua kwamba Virgil van Dijk amerejea kikosini.

„Virgil amerejea," kocha alithibitisha. „Alifanya mikimbio kadhaa uwanjani, alionekana kuwa mzuri tena. Kwa hiyo atarejea kikosini, amepona vizuri," alithibitisha Lijnders.

HABARI MICHEZO

# BENCHIKHA ATOA ONYO KWA WACHEZAJI WAVIVU, WASIO NA NIDHAMU KIKOSINI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, ametoa onyo kali kwa wachezaji wa timu hiyo akiwataka kujitoa na kujituma kwa ajili ya kuipambania nembo ya klabu hiyo na kuwawashia taa nyekundu wachezaji wavivu.

Benchikha amesema timu hiyo ina wachezaji wenye vipaji na uwezo mkubwa lakini baadhi yao wametawaliwa na uvivu wa mazoezi na kujituma uwanjani.

"Kuna wachezaji wana uwezo mkubwa na vipaji, lakini tatizo linakuja kwenye kujituma na kuipambania timu, kama kocha siwezi kuvumilia hali hii na nimewaambia wabadilike," alisema Benchikha.

Aidha, alisema hataweza kuvumilia kuona mchezaji anacheza chini ya kiwango kwa sababu atakuwa anakwamisha mipango yake na kile kinachotarajiwa na Wanasimba na wadau wa soka nchini.

Benchikha ametoa kauli hiyo kufuatia kuwapo kwa sakata la kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Clatous Chama kupelekea kusimamishwa kwa madai ya utovu wa nidhamu na kupelekwa kwenye kamati ya nidhamu ndani ya timu hiyo.

Simba ipo visiwani Zanzibar katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambapo Benchikha anayatumia kuandaa timu yake kwa ajilj ya michezo ijayo ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi.

Kocha huyo anatumia mashindano ya Mapinduzi pia kutengeneza muunganiko na kombinesheni ya wachezaji wapya waliosajiliwa katika kipindi hiki cha dirisha dogo.

Simba imewasajili Saleh Karabanka kutoka JKU FC ya Zanzibar, Ladack Chasambi kutoka MtibwaSugar na Babacar Sarr raia wa Senegal.

Benchikha alisema kuwa wachezaji wake wote wanapaswa kuwa kwenye daraja moja ambao wanatakiwa kuhakikisha wanajituma ndani ya timu yao na wala hataki kusikia kuna mchezaji mkubwa kuliko timu yenyewe.

"Sihitaji kuona mchezaji anajiona mkubwa kuliko timu jambo ambalo litaharibu na kuleta mvurugano kwa walio kwenye mstari wa timu, nataka kuona kila mchezaji anatimiza wajibu wake ili kufikia malengo yetu hasa kwenye ligi na michuano ya kimataifa, sitamvumilia mchezaji atakayeenda kinyume na hili," alisema Benchikha.

# Yanga yabakisha mataji matatu, yapoteza mawili

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imebakisha mataji matatu ambayo inaweza kuyapambania msimu huu, huku ikiwa imeshapoteza mawili mpaka sasa.

Kutolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Kombe la Mapinduzi Jumapili iliyopita kwa kufungwa mabao 3-1 dhidi ya APR ya Rwanda kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, mjini Zanzibar, kulimaanisha kuwa imepoteza taji la pili kati ya matano ambayo walikuwa wanawania msimu huu.

Tayari, Rais wa Klabu hiyo, Injinia Hersi Said, amemwambia Kocha Mkuu, Miguel Gamondi kuwaacha wachezaji ambao anaona hawawezi kumsaidia katika kufikisha malengo yake na ya klabu katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

"Mchezaji ambaye hakuonyesha kiwango chake katika michuano kama hiyo na kutupa ushindi sisi Wanayanga tuliomtuma, huyo mchezaji kwetu hawezi kuwa na nafasi tena, wapi sasa atatupa matokeo mazuri na kuonyesha kiwango chake kama kwenye mashindano kama ya mapinduzi ameshindwa?" alihoji Hersi na kuongezea,

"Mchezaji ambaye hajaweza kutimiza majukumu yake kwenye uwanja, huyo hafai kuwa na klabu yetu, kocha tumempa mamlaka ya kumwondoa yeyote ambaye anaona hatufai," alisema Rais huyo siku chache tu baada ya timu hiyo kutolewa kwenye michuano hiyo.

Yanga ilipoteza taji la kwanza ambalo ni Ngao ya Jamii, Agosti 13 mwaka jana kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga ilipofungwa kwa mikwaju ya penalti 3-1 dhidi ya watani zao wa jadi, Simba.

Ilikuwa ni baada ya suluhu ambapo timu hizo zilikwenda kwenye mikwaju ya penalti na Yanga kushindwa kuchukua taji hilo ambalo ilikuwa inalishikilia.

Kwa sasa Yanga inasaka mataji matatu ambayo ni ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Afrika inayoendelea huku timu hiyo ikiwa kwenye hatua ya makundi.

Katika hayo, Yanga inayashikilia mataji mawili ambayo ni ya Ligi Kuu na Kombe la FA iliyoyachukua msimu uliopita.

Ilitwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu wa 2022/23 kwa kukusanya pointi 76 kwa michezo 30 iliyochezwa na ilikuwa bingwa la Kombe la FA kwa kuifunga Azam FC mabao 1-0 katika mechi ya fainali iliyochezwa Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Juni 12 mwaka jana kwa bao la Kennedy Musonda.



Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akiwa mazoezini nchini Ivory Coast kujiandaa na Fainali ya Mataifa ya Afrika (AFCON) itakayoanza Januari 17. **PICHA: BINZUBEIRY**

# Utata Simba Queens, JKT

INATOKA UK. 24

kama klabu , watawala na wasimamizi wa mpira ili mpira wetu uzidi kuheshimika na kuwa na mvuto kwa watu.

Bwire alisema baada ya sakata hilo wanasubiri kuona taarifa rasmi watakayoletewa na baada ya hapo wataitazama na kuzungumza.

"Kama wametoa ushindi kwa wapinznai wetu, ngoja tusubiri na sisi tujiridhishe katika hilo ili tuje na kauli ambayo itakuwa sawasawa, "alisema Bwire.

Mmoja wa viongozi wa Bodi ya klabu ya Simba na mlezi wa Simba Queens, Asha Baraka alisema JKT waliogopa ,mziki' wao ndio maana wamekimbia huku wakiitaka TFF kuwapa pointi zao tatu.

"Timu zote tulipewa taarifa mapema ya mchezo huu kufanyika Chamazi na hata kwenye mkutano wa awali kabla ya mechi timu zote zilikuwepo na zikakubalina sasa sijui wenzetu wamebadilikaje, ila najua walituogopa.

"Tutawaandikia TFF barua watupe pointi tatu ambazo tunazingoja hayo mambo ya kanuni watajua wenyewe wanaoendesha mpira wao, sisi tunachojua tumefika uwanjani kwa kufuata taratibu zote na tumetumia gharama hivyo tunastahili haki yetu, "alisema Asha.

Mara ya mwisho timu hizo zilikutana kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii Desemba 12 wakufungua msimu mpya wa Ligi Kuu ya wanawake ambapo Simba ilishinda kwa mikwaju ya penalti 5-4 baada ya kumaliza dakika tisini wakiwa wamefungana bao 1-1.

Mpaka sasa JKT Queens inaongoza ligi kwa tofauti ya magoli ya kufunga na kufungwa wakiwa na pointi tisa sawa na Simba wanaoshika nafasi ya pili.

# Wachezaji Stars kujituma

INATOKA UK. 24

kushirikiana kwa pamoja tutafikia malengo yetu, mara hii hatutaki kuishia hatua ya makundi angalau tufike hata robo fainali. Tunataka kuweka rekodi mpya, tumechoka kuishia hatua ya makundi ya michuano hii, kila mchezaji anatamani kufanya vizuri, kwa msaada wa Mungu na maombi ya Watanzania naamini tutafikia malengo yetu," alisema Samatta.

Aliongeza kuwa wanatambua wanakutana na timu nzuri katika kundi lao na wanaiheshimu kila timu kwenye kundi hilo lakini wajipanga kushindana kupata nafasi ya kusonga mbele.

"Ukiliangalia kundi tulilopo sio jepesi, tunatakiwa kuwaheshimu wapinzani wetu, kinachotakiwa ni kujiandaa kwa ajili ya kushindana na sio kushiriki," alisema Samatta.

Michezo
Alhamisi Januari 11, 2024
Nipashe

## Henderson awa lulu Ligi za Ulaya

UKURASA 21






Wachezaji wa Simba (kushoto) wakiwa kwenye Uwanja wa Azam Complex juzi wakifanya mazoezi mepesi kujiandaa na mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya JKT Queens, kulia wapinzani wao wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo kwa ajili ya mchezo huo. **PICHA: MTANDAO**

# KAMATI YA TFF KUAMUA UTATA SIMBA QUEENS, JKT

●●● Ni baada ya mchezo wao kutofanyika kutokana na kila timu kwenda kwenye uwanja wake, kiongozi TFF anena...

**Na Oliver Albert**

KAMATI ya mashindano ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) ndio itatoa uamuzi wa nani alikuwa sahihi katika mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake kati ya JKT Queens dhidi ya Simba Queens.

Timu hizo zilikuwa zicheze mechi yao ya Ligi Kuu Bara juzi lakini ikashindwa kufanyika baada ya kila timu kwenda kwenye Uwanja wake na kuzua mshangao kwa wadau wa soka.

JKT Queens ambao ndio walikuwa wenyeji wa mchezo huo wao walienda kwenye uwanja wao wa nyumbani wa Meja Jenerali Isamuhyo uliopo Mbweni wakiwasubiri wageni wao Simba lakini wapinzani wao walikuwa katika uwanja wa Azam Complex Chamazi pamoja na waamuzi wakifuata maagizo ya TFF ambao walitaka mechi hiyo ifanyike huko.

Saa 10 jioni ambapo ndio muda uliopangwa mchezo huo kuanza, waamuzi waliikagua Simba Queens waliokuwepo uwanjani na kisha kusubiri dakika 30 bila JKT Queens kutokea na kuumaliza mchezo.

Mkurugenzi wa wa mashindano wa TFF, Salum Madadi aliliambia gazeti hili kuwa yote yaliyotokea wameyaona na kuyasikia hivyo wanasubiri kamati ikae na kufanya uamuzi.

"Kama TFF tumeshapokea ripoti ya mchezo kutoka kwa wahusika na tumeipeleka kwenye kamati ya mashindano husika ambayo itakaa na kutoa uamuzi hivyo watu wasubiri kamati itafanya nini, "alisema Madadi.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Idara ya Habari wa timu za soka za JKT, Masau Bwire alisema wanachojua walikuwa sahihi kulingana na kanuni inavyosema.

"Kanuni ya 9 kifungu cha pili (ii) kinazungumzia uwanja na mabadiliko yake na kinasema...., "Kama kuna mabadiliko ya uwanja wa kutumika katika kucheza mpira kuwepo na sababu nzito sana za muhimu lakini taarifa za mabadiliko hayo zitolewe angalau siku saba kabla",

"Ukiangalia hiyo barua ambayo sisi hatukupata hata kwenye barua pepe yetu haipo na hatuna popote na wao walidai iliandikwa tarehe 4 Januari 2024 na mechi inachezwa Januari 9, sasa ukitazama hapo kuna siku tano tu za taarifa nje ya utaratibu wa kikanuni, "alisema Bwire na kuongeza;

"Usitazame tu kwamba timu imefanya nini bali tutazame je kanuni imezingatiwa kwani kanuni hizi tunazoziweka ni vizuri tukazifuata sisi

INAENDELEA UK. 23

# Amrouche awataka wachezaji Stars kujituma

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya soka ya Taifa ,Taifa Stars', Adel Amrouche amewataka wachezaji wa timu hiyo, kucheza kwa bidii na kuonyesha vipaji vyao katika mechi ya kwanza ya Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) dhidi ya Morocco itakayochezwa kwenye Uwanja wa San Pedro nchini Ivory Coast, Januari 17.

Fainali hizo za AFCON zinatarajiwa kuanza Januari 13 hadi Februari 11, mwaka huu huku Tanzania iliyopo kwenye Kundi F pamoja na Dr Congo na Zambia ikianza kufungua dimba kwa kucheza na Morocco.

Akizungumza na Nipashe jana, Amrouche alisema amefanyia kazi mapungufu ya kikosi chake katika mechi iliyopita ya kirafiki dhidi ya Misri na sasa amewataka wachezaji kupambana katika michezo iliyopo mbele yao kuanzia dhidi ya Morocco.

Alisema bado hajashtushwa na matarajio ya kukabiliana na wapinzani wakubwa, anaelewa changamoto iliyo mbele yao kwa kusahihisha makosa yao kabla ya kuvaana na Morocco.

"Hii ni fursa kubwa kwa wachezaji kuyatumia mashindano haya ikiwa ni sehemu ya kuonyesha uwezo mzuri lakini lengo letu la msingi ni kutoa uwezo wetu na kupata matokeo bora na kuacha kila kitu uwanjani, alisema Amrouche na kuongeza,

Mashindano haya yanatoa nafasi ya kujitangaza kwa kila mchezaji, lakini pia kupata fursa ya kucheza na timu bora zaidi barani Afrika, nina matumaini makubwa ya kufanya vizuri kulingana maandalizi ya timu tuliyofanya, wachezaji wakitenda vizuri na kuhamisha ya mazoezi na kupeleka uwanjani watafanya vizuri zaidi katika makundi," alisema Amrouche.

Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta alisema , wamekuwa wakishiriki tu mashindano hayo, sasa hivi wamejipanga kuhakikisha wanafuzu hatua inayofuata.

"Tumejiandaa vizuri, tunaamini kwa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >